


VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

Mwaka wa Pili

Kitabu cha Nne



**BIBLIA,
KITABU CHA DAIMA**

VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

Mwaka wa Pili

Kitabu cha Nne

Africa Coordinated Curriculum for
Bible Study

J2 - 4P

Published and printed by
Baptist Publications House
Box 30370, Likoni Rd., Nairobi

VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

Mwaka wa Pili

Kitabu cha Nne

Y A L I Y O M O

<u>Sura</u>	<u>Ukurasa</u>
Ujumbe Kwa Mwanafunzi.....	4
1. Jinsi Biblia Ilivyoandikwa.....	5
2. Biblia Inasema Nasi.....	13
3. Kijana Aliyependa Kitabu cha Mungu.....	22
4. Sheria ya Mungu Kwa Mwili Wetu..	30
5. Jinsi Yesu Alivyotumia Biblia...	39
6. Watendaji wa Neno.....	46
7. Wakati Mungu Alipotoa Sheria Zake.....	54
8. Kuishi Kwa Sheria za Mungu.....	61
9. Yesu Aeleza Sheria za Mungu.....	69
10. Wakati Tunapokosa Kutii Sheria za Mungu.....	76
11. Njia ya Kuwa na Furaha.....	87
12. Kipawa Kikuu.....	95
13. Tunu Zangu Kwa Mungu.....	103

UJUMBE KWA MWANAFUNZI

Je! Biblia ina maana gani kwako?
Je! unao wakati maalum kila siku kusoma Biblia? Biblia ni ujumbe wa Mungu kwetu. Ni Kitabu Kitakatifu. Kina ujumbe wa uzima wa milele ambao Mungu anawapa wale wanaomwamini Mwanawe Yesu Kristo kama Mwokozi wao.

Tunaweza kusema kwamba Biblia ni Kitabu kinachotuonyesha njia ya kuishi maisha mema. Ni kitabu cha daima, si cha Shule ya Jumapili na mahubiri ya ibada peke yake.

Katika masomo yetu matano yanayofuata, tutajifunza jinsi tulivyoweza kuwa na Kitabu hiki cha Mungu. Tutaona kwamba ni Kitabu kinachotupasa kukipenda na kukijifunza. Tutaona kwamba kujua mambo yake pekee hakutoshi. Ni lazima tufanye mambo ambayo kinasema.

Tunaomba kwamba utakua katika upendo wako kwa Neno la Mungu. Tunaomba kwamba utakua katika ufahamu wako juu ya ujumbe wa Neno hilo. Ufahamu huo wako utakuongoza kila siku na utakuonyesha mambo yaliyo haki na yale yasiyo haki. Utaona jinsi wengine wametumia Neno la Mungu kama kiongozi wao wanayefuata mfano wake katika maisha yao.

JINSI BIBLIA ILIVYOANDIKWA

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 24:1-4, 12 na 18; 32:1, 7, 15, 16 na 19, 34:1, 4 na 29; 40:20

Je! unajua jinsi tulivyopata Biblia yetu? Ulijua kwamba vitabu vyote vya Biblia havikuandikwa mara moja na mtu mmoja?

Mungu alitoa Neno lake kwa watu wengi mbalimbali. Watu hawa waliandika maneno ambayo Mungu alisema. Ilichukua miaka mingi sana kuandika kitabu cha Biblia.

Mtu wa kwanza ambaye Mungu alitumia kuandika Biblia alikuwa Musa. Musa aliwaongoza Waisraeli kutoka katika nchi ya Misri. Waisraeli hao walikuwa wengi sana. Hawakuwa na sheria yo yote iliyoandikwa kuwaonyesha jinsi Mungu alivyowataka kuishi.

Wakati Waisraeli walipokuwa wakisafiri jangwani, waligombana wenyewe. Walimnug'unikia Musa juu ya chakula na maji. Ilionekana kwamba walimsahau Mungu.

Wakati Waisraeli walipofika katika Mlima wa Sinai, walipiga hema zao. Mungu alimpa Musa maongozi maalum. Alimwambia kupanda Mlima huo wa Sinai.

Musa alipanda Mlima huo wa Sinai, na Mungu alisema naye kuhusu sheria zake. Aliandika maneno yote ambayo Mungu alisema ili angeweza kuwaambia wana wa

Israeli. Kisha Mungu mwenyewe aliandika Amri zake Kumi katika mbao za mawe.



Baada ya Musa kukaa mlimani siku arobaini mchana na usiku, alibeba mbao zile ambazo Mungu aliandika amri zake, akashuka. Mbao hizo angewapa Waisraeli ili wangepeweza kujua jinsi ya kuishi vyema pamoja kwa furaha. Mungu alimpa Musa sheria nyingine nyingi pia kuwao-ngoza.

Wakati Musa alipokaribia kambi ya Waisraeli, alisikia watu wakiimba na wakipiga kelele. Alijiharakisha kwenda kuona kitu kilichokuwa kikifanyika. Aliwakuta watu wakiimba na kuabudu sanamu ya ndama.

Musa alipoona matendo hayo, alikasirika sana. Alitupa mbao zile mikononi mwake, akazivunja vipande vidogo. Kisha alitwaa sanamu ile ya ndama, akaiharibu.

Musa alikasirishwa sana na matendo ya Waisraeli. Aliwaombea, tena alimsihi Mungu kuwasamehe dhambi zao.

Mungu alimwambia Musa tena kupanda Mlima wa Sinai. Alimwambia kuleta mbao nyingine mbili za mawe kama zile za kwanza alizovunja. Musa alichukua mbao nyingine mbili, akapanda Mlima wa Sinai. Tena alikaa huko siku arobaini usiku na mchana.

Musa aliposhuka mlimani wakati huu, Haruni na Waisraeli walikuwa wakimngojea. Walimsikiliza wakati alipowasomea Amri Kumi za Mungu ambazo Mungu aliziandika tena katika mbao za mawe.


Kisha Musa alitia mbao zile za mawe ndani ya sanduku lililoitwa Sanduku la Agano. Mbao zile zilikuwa salama ndani Sanduku lile la Agano wakati Waisraeli walipokuwa wakisafiri kwenda Nchi ya Ahadi.



Tumekwisha kuona ya kwamba Mungu mwenyewe ndiye aliyeandika kwanza Amri zake Kumi katika mbao mbili za mawe. Kulikuwa na njia nyingine ambayo Neno la Mungu liliandikwa. Liliandikwa kwenye ngozi ya mnyama iliyokunjwa. Mungu aliwa-

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

pa manabii Neno lake.
Manabii hao waliwaambia
waandishi maneno Mungu
aliyoyasema. Kisha wa-
andishi waliandika
maneno hayo kwenye hati
ya kuviringisha.



Agano la Kale liliandikwa katika
lugha ya Kiebrania. Agano Jipya liliandi-
kwa katika lugha ya Kiyunani. Ni ajabu
sana kufikiria mpango ambao Mungu alitu-
mia kutupa Neno lake. Tuombe sasa tuki-
mshukuru Mungu kwa Neno lake tuliloandi-
kiwa.

KAZI YA KUFANYA:

Siku ya leo umejifunza jinsi Biblia
iliandikwa. Jaribu kuona kama unaweza
kukumbuka mambo mengi ya somo hili.
Andika majibu yako katika mistari iliyo-
achwa.

1. Mungu alitoa Amri zake Kumi kwa
mtu mmoja aliyeitwa _____.
2. Amri zile Kumi ziliandikwa katika
mbao za _____.
3. Amri zile ziliandikwa na _____
mwenyewe.
4. Musa alitia mbao zile za mawe ndani
ya sanduku lililoitwa _____ la
_____.

5. Mungu alisema na wajumbe pia wali-
oitwa _____.
6. Ujumbe huu wa Mungu uliandikwa
na waandishi kwenye ngozi ya mnyama
iliyokitwa _____ ya _____

Biblia yetu iliandikwa katika lugha
mbili. Andika majibu katika mistari ya
sentensi zifuatazo hapo chini.

1. Agano la Kale liliandikwa katika
lugha ya _____.
2. Agano Jipya liliandikwa katika
lugha ya _____.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

*"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu,
lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwa-
onya watu makosa yao, na kwa kuwa-
ongoza, na kwa kuwaadibisha katika
haki."* 2 Timotheo 3:16

Kifungu chetu cha kukumbuka kinatwa-
mbia kwamba Mungu aliwaongoza watu kwa
Roho yake kuandika ujumbe wake kwetu.
Neno lake litatufundisha mambo yaliyo
kweli. Litatuonyesha mambo ambayo ni
makosa maishani mwetu.

Neno la Mungu litatufundisha kuwa
Wakristo wanaompendeza Bwana. Ni nuru
inayotuongoza. Je! unaruhusu Neno la
Mungu kuwa nuru kukuongoza katika maisha
yako?

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

MANENO YA KUJIFUNZA:

ndama.....mtoto wa mnyama,
hasa wa ng'ombe.
Sanduku la Agano....sanduku ambalo mbao
zile mbili za mawe
ambazo Mungu aliandi-
ka sheria zake zili-
wekwa ndani.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Kutoka 24:1-4, 12, 18

Kisha BWANA akamwambia Musa, kweeni wewe, na Haruni, na Nadabu, na Abihu, na watu sabini wa wazee wa Israeli, mkamfikilie BWANA; mkasujudie kwa mbali; (2) na Musa peke yake ndiye atakayekaribia karibu na BWANA; lakini hao hawatakaribia karibu; wala hao watu hawatakwea pamoja naye. (3) Musa akaenda akawaambia watu maneno yote ya BWANA, na hukumu zake zote; watu wote wakajibu kwa sauti moja, wakasema, Maneno yote aliyoyanena BWANA tutayatenda. (4) Basi Musa akayaandika maneno yote ya BWANA, akaondoka asubuhi na mapema, akajenga madhabahu chini ya mlima, na nguzo kumi na mbili, kwa hesabu ya kabila kumi na mbili za Israeli.

(12) BWANA akamwambia Musa, Njoo huku juu kwangu mlimani, uwe huku; nami nitakupa mbao za mawe na ile sheria na hiyo amri niliyoandika ili uwafundishe. (18) Musa akaingia ndani ya ile wingu, akapanda mlimani; Musa akawa humo katika ule mlima siku arobaini, mchana na usiku.

Kutoka 32:1, 7, 15, 16, 19

Hata watu walipoona ya kuwa Musa amekawia kushuka katika mlima, wakakusanyana wakamwendea Haruni, wakamwambia, Haya! katufanyizie miungu itakayokwenda mbele yetu, kwa maana Musa huyo aliyetutoa katika nchi ya Misri hatujui yaliyompata.

(7) BWANA akamwambia Musa, Haya! shuka; kwa maana watu wako uliowatoa katika nchi ya Misri wamejiharibu nafsi zao.

(15) Basi, Musa akageuka akashuka katika mlima, na zile mbao mbili za mawe mikononi mwake; mbao zilizoandikwa pande zote mbili, upande huu na upande huu ziliandikwa. (16) Na zile mbao zilikuwa kazi ya Mungu, nayo maandiko yalikuwa maandiko ya Mungu, yaliyochorwa katika zile mbao. (19) Hata alipoyakaribia marago akaiona ile ndama, na ile michezo. Hasira ya Musa ikawaka, akazitupa zile mbao mikononi mwake, akazivunja chini ya mlima.

Kutoka 34:1, 4, 29

Kisha BWANA akamwambia Musa, Chonga mbao mbili za mawe mfano wa zile za kwanza; nami nitaandika juu ya mbao hizo maneno hayo yaliyokuwa juu ya mbao za kwanza, hizo ulizozivunja. (4) Naye akachonga mbao mbili za mawe mfano wa zile za kwanza; na Musa akainuka na mapema asubuhi, naye akakwea katika mlima wa Sinai, kama BWANA alivyomwamuru, akazichukua hizo mbao mbili za mawe mikononi mwake.

(29) Hata ikawa, Musa aliposhuka katika mlima Sinai, na zile mbao mbili za ushuhuda zilikuwa mkononi mwa Musa, hapo aliposhuka katika mlima, Musa haku-jua ya kuwa ngozi ya uso wake iling'aa kwa sababu amesema naye.

Kutoka 40:20

Akautwaa ule ushuhuda, akautia ndani ya sanduku, akaiweka miti ya kuchukulua juu ya sanduku, akakiweka kiti cha rehema juu ya sanduku.



BIBLIA INASEMA NASI

MASOMO YA BIBLIA: Yeremia 36:1,2;
2 Petro 1:21; Waebrania 4:12;
Yohana 20:30, 31; Isaya 40:8; Zaburi
19:7-10; Luka 21:33

Je! umepata kufikiria jinsi Mungu alivyo? Umepata kutamani Mungu kusema nawe?

Mungu anataka kusema nawe kila siku. Anakupenda na ana ujumbe mwingi kwako katika Biblia ambalo ni Neno lake.

Biblia ni kitabu cha ajabu! Hakuna kitabu kingine ulimwenguni mwote ambacho ni kama Biblia. Vitabu vingine vyote vimeandikwa na watu. Lakini Mungu mwenyewe ndiye aliyeandika Biblia. 2 Timotheo 3:16 inatwambia kwamba maandiko yote yenye pumzi ya Mungu yanafaa kwa mafundisho. Hii maana yake ni ya kwamba Mungu aliwaambia watu mambo ya kuandika.

Mungu alitumia watu wengi kuandika Neno lake. 2 Petro 1:21 inatwambia kwamba watu hawa walinena wakiongozwa na Roho Mtakatifu. Je! unajua majina ya baadhi ya watu hawa? Jaribu kuona kama unaweza kukumbuka majina mengi.

Je! umepata kufikiria jinsi kitabu hiki cha zamani sana kinaweza kusema nawe leo? Ni kweli kwamba maneno unayosoma ndani ya Biblia yaliandikwa zamani sana. Lakini Mungu ni kama jana na leo na sikuzote. Habadiliki. Neno lake pia halibadiliki. Ameahidi kwamba Biblia

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

ambayo ni Neno lake itadumu milele! Hai-
tapita kamwe! (Soma Luka 21:33.)

Biblia yetu imegawanywa katika
sehemu mbili, Agano la Kale na Agano
Jipya. Agano la Kale lina vitabu thela-
thini na tisa. Agano Jipya lina vitabu
ishirini na saba. Neno "agano" maana
yake ni "ahadi" au "mapatano." Biblia
imejaa ahadi na mapatano ya Mungu nasi.

Je! unajua majina ya vitabu vingapi
vya Biblia? Ikiwa huyajui, ujifunze ili
utaweza kuyajua yote wakati utakapomaliza
masomo haya. Hapo chini kuna orodha ita-
kayokusaidia kujifunza majina ya vitabu
vya Biblia.

AGANO LA KALE

Mwanzo	Mithali
Kutoka	Mhubiri
Mambo ya Walawi	Wimbo ulio Bora
Hesabu	Isaya
Kumbukumbu la	Yeremia
Torati	Maombolezo
Yoshua	Ezekieli
Waamuzi	Danieli
Ruthu	Hosea
1 Samweli	Yoeli
2 Samweli	Amosi
1 Wafalme	Obadia
2 Wafalme	Yona
1 Mambo ya Nyakati	Mika
2 Mambo ya Nyakati	Nahumu
Ezra	Habakuki
Nehemia	Sefania
Esta	Hagai
Ayubu	Zekaria
Zaburi	Malaki

AGANO JIPYA

Mathayo	1 Timotheo
Marko	2 Timotheo
Luka	Tito
Yohana	Filemoni
Matendo	Waebrania
Warumi	Yakobo
1 Wakorintho	1 Petro
2 Wakorintho	2 Petro
Wagalatia	1 Yohana
Waefeso	2 Yohana
Wafilipi	3 Yohana
Wakolosai	Yuda
1 Wathesalonike	Ufunuo
2 Wathesalonike	

Katika somo lililopita tulijifunza kwamba Agano la Kale liliandikwa katika lugha ya Kiebrania. Agano Jipya liliandi- kwa katika Lugha ya Kiyunani. Sasa kuna tafsiri ya Biblia na sehemu zake katika lugha zaidi ya 1200. Inatupasa kuwa na shukrani kwa sababu tunayo Biblia iliyo- tafsiriwa katika lugha yetu!

Biblia inatwambia kwamba inatupasa kukua katika neema na katika kumjua Bwana wetu Yesu Kristo. (Soma 2 Petro 3:18.) Tunawezaje kukua katika kumjua Yesu? Tunakua kwa kujifunza Biblia. Ni lazima tusome Neno la Mungu kila siku.

Je! ulikula chakula kila siku wiki iliyopita? Kwa nini? Ulikula chakula kwa sababu ulikuwa na njaa. Ikiwa hungali- kula, ungalikuwa mnyonge. Labda ungali- kuwa mgonjwa kama hungalikula chakula.



Tutakuwa wadhaifu sana katika maisha yetu ya kiroho ikiwa hatusomi Neno la Mungu. Hata tutakuwa wagonjwa kiroho. Mungu anatutaka sisi kuwa watiifu na waaminifu kwake. Ni lazima tusome Neno lake ili tuweze kujua jinsi ya kumtii. Inatupasa kutii kila amri ya Mungu.

Mungu ana ahadi nyingi kwetu. Anaitwambia kwamba atatutunza sikuzote. Je! ni ahadi ngapi unazojua? Soma vifungu vifuatavyo. Ni baadhi ya ahadi za ajabu za Mungu kwetu.

"Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu." (Wafilipi 4:13)

"Na Mungu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake..." (Wafilipi 4:19)

"Bwana yuko upande wangu, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini?" (Zaburi 118:6)

"Mungu, njia yake ni kamilifu, ahadi ya Bwana imehakikishwa, yeye ndiye ngao yao wote wanaomkimbilia." (Zaburi 18:30)

Je! unaogopa usiku? Ikiwa unaogopa, hapa kuna ahadi kwako:

"Nalijilaza nikalala usingizi, nika-amka, kwa kuwa Bwana ananitegemeza. Sita-yaogopa makumi elfu ya watu, waliojipanga juu yangu pande zote." (Zaburi 3:5,6)

Neno la Mungu linatufundisha ukweli wa Mungu. Linatufundisha kwamba Yesu ndiye njia na kweli na uzima. (Soma Yohana 14:6.) Tunajifunza kwamba tunapoliita jina la Bwana, tutaokolewa. (Soma Warumi 10:13.) Tunajifunza kwamba tunapoungama dhambi zetu kwa Mungu, atatusamehe. (Soma 1 Yohana 1:9.)

Neno la Mungu hutuonyesha dhambi zetu. Linasema, "Wapendeni adui zenu...." (Mathayo 5:44) Ikiwa unawachukia adui zako, unatenda dhambi.

Neno hilo linasema, "Enyi watoto, watiini wazazi wenu...." (Waefeso 6:1) Msipowatii wazazi wenu mnatenda dhambi.

Ndiyo, Neno la Mungu linasema nasi. Ulisome kila siku kama unavyokula chakula. Hii ndiyo njia ya kukua katika kumjua Bwana Yesu Kristo.

KAZI YA KUFANYA:

Je! ulijifunza Biblia kadiri gani leo? Hapa kuna maswali ya kukujaribu. Tazama kama unaweza kupata jibu kweli la kila swali.

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

Chini ya maswali yafuatayo kuna namba. Chagua namba ambayo ni jibu la swali na kuliandika katika mstari ulio mwishoni mwa swali hilo.

1. Kuna sehemu ngapi katika Biblia yetu? _____
2. Kuna vitabu vingapi katika Agano la Kale? _____
3. Kuna vitabu vingapi katika Agano Jipya? _____
4. Ni lugha ngapi zilizotumiwa kuandika Biblia? _____

(Namba: 2, 27, 2, 39.)

Kuna ahadi za ajabu zilizoandikwa katika somo hili la leo. Chagua ahadi ile unayoipenda sana. Uandike katika mistari hiyo hapo chini.

Kariri ahadi hiyo uliyoandika. Iseme kila siku. Ni ahadi ya Mungu kwako.


KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Bali Neno la Bwana hudumu hata milele. Na Neno hilo ni neno lile jema lililohubiriwa kwenu."

1 Petro 1:25

Ni ngumu sana kwetu kufahamu maana ya neno "milele." Kitu ambacho ni "milele" hakitakuwa na mwisho. Tazama mahali ulipo. Siku moja, vitu unavyoviona hapo vitaharibiwa. Nguo huzeeka. Viatu huisha. Wino wa kalamu yako huisha. Kalamu ya penseli unayoandikia pia huisha. Mfuko wa unga unaotumia humalizika baada ya siku chache tu.

Tazama picha ifuatayo. Weka herufi "X" katika vitu ambavyo vitaharibiwa. Chora mviringo kwa vitu ambavyo vitadumu milele.



BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

Mvua inapokosa kunyesha, maji ya mito hukauka. Mvua inaponyesha, unalima shamba lako kwa sababu majani yanaendelea kukua. Kila mwaka ni lazima baba yako kulima. Kulima mara moja tu hakutadumu milele! Ni kazi ya kufanya kila mwaka.

Maua humea na kupendeza kwa muda mfupi tu. Kisha hunyauka. Lakini kuna kitu kimoja kinachodumu milele. Ni Neno la Mungu. Unapokariri kifungu cha Biblia, unajifunza kitu ambacho ni kweli daima. Je! unashukuru kwamba una Neno la Mungu kujifunza na kuliweka moyoni mwako?

MANENO YA KUJIFUNZA:

nyauka.....kukauka.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Yeremia 36:1,2

Ikawa katika mwaka wa nne wa Yehoyakimu, mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda, neno hili likamjia Yeremia, kutoka kwa BWANA, kusema, (2) Twaa gombo la chuo, ukaandike ndani yake maneno yote niliyo-kuambia juu ya Israeli, na juu ya Yuda, na juu ya mataifa yote, tangu siku ile niliponena nawe, tangu siku za Yosia, hata siku hii ya leo.

2 Petro 1:21

Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu wali-nena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

Waebrania 4:12

Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.

Yohana 20:30,31

Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. (31) Lakini hizi zimeandikwa; ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake.

Isaya 40:8

Majani yakauka, ua lanyauka; Bali neno la Mungu wetu litasimama milele.

Zaburi 19:7-10

Sheria ya BWANA ni kamilifu, Huibu-rudisha nafsi. Ushuhuda wa BWANA ni amini, Humtia mjinga hekima. (8) Maagizo ya BWANA ni ya adili, Huufurahisha moyo. Amri ya BWANA ni safi, Huyatia macho nuru. (9) Kicho cha BWANA ni kitakatifu, Kinadumu milele. Hukumu za BWANA ni kweli, Zina haki kabisa. (10) Ni za kutamanika kuliko dhahabu, Kuliko wingi wa dhahabu safi. Nazo ni tamu kuliko asali, Kuliko sega la asali.

Luka 21:33

Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe.

KIJANA ALIYEPENDA KITABU CHA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: 2 Timotheo 1:1-14

Je! unaweza kukumbuka wakati wako wa kwanza uliposikia Neno la Mungu? Unakumbuka wakati ulipoanza kusoma Neno la Mungu wewe mwenyewe? Ikiwa umekuwa ukihudhuria Shule ya Jumapili na kanisa kwa muda mfupi tu, utaweza kukumbuka. Ikiwa unakaa katika nyumba ya Kikristo, basi, pengine hutaweza kukumbuka wakati wako wa kwanza uliposikia Neno la Mungu.

Siku ya leo tunajifunza juu ya kijana mmoja mhubiri anayeitwa Timotheo. Mama yake alimfundisha Neno la Mungu tangu wakati alipokuwa kijana mdogo. Alikariri vifungu vingi vya Biblia. Labda hangeweza kukumbuka wakati wa kwanza aliposikia habari za Mungu.

Somo letu la Biblia leo linatoka katika barua ya pili ya Paulo kwa Timotheo. Hebu tuone mambo tunayoweza kujifunza juu ya Timotheo katika barua hii.

Kwanza, tunajifunza kwamba Paulo alimpenda Timotheo sana. Katika 2 Timotheo 1:2, Paulo anamwita Timotheo, "mwanangu mpendwa." Ilikuwa baraka kubwa kwa Timotheo kupendwa na mtume Paulo!

Lakini kulikuwa na sababu iliyomfanya Paulo kumpenda Timotheo sana. Timotheo alijifunza kumpenda Mungu na kuwa na imani kwake wakati alipokuwa

KIJANA ALIYEPENDA KITABU CHA MUNGU

mdogo. Paulo alimpenda Timotheo kwa sababu Timotheo alimpenda Mungu sana.

Timotheo alibarikiwa katika njia nyingine kubwa. Alikuwa na mama na nyanya waliomwabudu Mungu. Walikuwa Wayahudi waaminifu. Mara kwa mara wakati alipokuwa mdogo, Eunike mamaye na Loisi nyanyaye walimfundisha Neno la Mungu. Timotheo, akiwa kama kijana Myahudi mwaminifu, alikwisha kukariri sana Neno la Mungu.



Biblia ambayo Timotheo alijifunza ilikuwa tofauti na Biblia zetu leo. Haikuwa na Agano Jipya. Haikuwa kama kitabu hiki tulicho nacho.

Je! unakumbuka mambo uliyojifunza katika somo la kwanza kuhusu njia mbali-
mbali ambayo Neno la Mungu liliandikwa zamani? Liliandikwa katika hati ya kuviringisha iliyotengenezwa kwa ngozi za kondoo au za mbuzi. Maneno yaliandikwa kwa mkono. Ngozi hizo zilikunjwa. Ilichukua muda mrefu sana kuandika Neno la Mungu katika hati za kuviringisha.

Timotheo hakuwa na Agano Jipya la kusoma kwa sababu lilikuwa bado kuandikwa. Lakini alijua mambo ambayo Agano la Kale lilisema juu ya Yesu kuja.

Kisha wakati Timotheo aliposikia kwamba Yesu, Masihi alikuja, aliamini. Alikumbuka mafundisho ya Agano la Kale aliyojifunza wakati alipokuwa kijana mdogo. Aliamini kwamba unabii wa Isaya juu ya Masihi kuja ulitimilizwa. Alimwamini Yesu kama Mwokozi wake.

Siku moja, Paulo alitembelea kikundi cha waamini mjini Listra. Waamini hao walimwambia habari za Timotheo. Walisema kwamba Timotheo alikuwa mfuasi mwaminifu wa Yesu. Paulo alikata shauri kwamba yeye pamoja na Sila wangemchukua Timotheo katika safari yao ya pili ya umisheni. Hakika, Timotheo alikuwa kijana mwenye furaha wakati aliposikia habari hiyo!

Timotheo alikuwa mfuasi mwaminifu wa Yesu kwa sababu alijifunza Neno la Mungu kutoka wakati alipokuwa kijana mdogo. Alijifunza ahadi na amri za Mungu. Aliamini ahadi hizo na alitii amri za

KIJANA ALIYEPENDA KITABU CHA MUNGU

Mungu. Sasa Mungu alimbariki kwa kumruhusu kumsaidia Paulo katika kazi yake.

Je! Timotheo angaliweza kuwa mfuasi mwaminifu wa Yesu kama hangalijifunza Neno la Mungu? La, kwa sababu hatuwezi kujua jinsi ya kuwa waaminifu na watiifu kwa Mungu kama hatujui Neno lake.

Ukijifunza Neno la Mungu kila siku, utakua katika ujuzi wako kumjua Yesu.. Utakuwa Mkristo mwenye nguvu wakati unapofuata amri zake.

Mungu anakutaka wewe kuwa shahidi wake mwaminifu nyumbani mwenu au shuleni. Ameahidi kukusaidia kwa sababu huwezi kufanya hivyo wewe mwenyewe bila msaada wake. Kabla Yesu kurudi mbinguni, aliwahidi wanafunzi wake ahadi hii: "...tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari." (Mathayo 28:20)

Ahadi hii ni ya ajabu mno! Timotheo alikuwa mwaminifu. Aliamini ahadi za Mungu. Tuombe ili kila mmoja wetu atakuwa mwaminifu kama Timotheo. Tuliweke Neno la Mungu mioyoni mwetu kama tunavyofundishwa na kifungu chetu cha kukumbuka.

KAZI YA KUFANYA:

Je! unaweza kukumbuka kadiri gani habari juu ya Timotheo katika somo hili la leo? Tazama kama unaweza kujibu maswali yafuatayo hapo chini. Chora mistari kutoka kwa maneno upande wa kushoto hadi

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

kwa yale upande wa kulia ambayo ni sawa:

Mama ya Timotheo alikuwa	aliamini Neno la Mungu.
-----------------------------	----------------------------

Nyanya ya Timotheo alikuwa	"Mwanangu Mpe- ndwa"
-------------------------------	-------------------------

Paulo alimwita Timotheo	Hati ya kuviri- ngisha.
----------------------------	----------------------------

Biblia Timotheo aliyojifunza inaitwa	Eunike.
--	---------

Paulo alisikia habari za Timotheo mjini	Loisi
---	-------

Paulo alipokutana na Timotheo ali- kuwa pamoja na	Sila
---	------

Wakati Paulo ali- pokutana na Timotheo alikuwa katika safari yake ya pili ya	Umisheni
--	----------

Timotheo alikuwa mwanafunzi mwami- nifu kwa sababu	Listra
--	--------

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

*"Basi usiuonee haya ushuhuda wa
Bwana....." 2 Timotheo 1:8*

KIJANA ALIYEPENDA KITABU CHA MUNGU

Je! unataka kumtii Mungu? Inatupasa kumtii kwa sababu tunampenda. Alitupa amri zake kwa sababu anatupenda. Je! ume-pata kumwambia mtu mwingine habari za Yesu? Yesu anakutaka wewe kuwaambia watu wengine habari zake. Labda unaweza kuwa na rafiki ambaye hajasikia habari za Yesu. Ukiomba, atakusaidia kujua mambo ya kusema.

Ukitaka kumtii Mungu ni lazima ujue amri zake. Unajifunza amri zake kwa kuso-ma Neno lake. Walakini, ni muhimu kuka-riri vifungu vya Biblia. Tunapojua jambo ambalo Mungu anatutaka sisi kufanya, ni lazima tufanye jambo hilo. Kufanya jambo hilo kunampendeza Mungu. Anatutaka sisi kujifunza vifungu vingi tunavyoweza kwa moyo.

MANENO YA KUJIFUNZA:

(Andika maneno yako ya kujifunza hapa.)

VIFUNGU VYA BIBLIA:

2 Timotheo 1:1-14

Paulo , mtume wa Kristo Yesu, kwa mapenzi ya Mungu; kwa ajili ya ahadi ya uzima ulio katika Kristo Yesu; (2) kwa Timotheo, mwanangu mpendwa. Neema na iwe kwako, na rehema, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Kristo Yesu Bwana wetu.

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

(3) Namshukuru Mungu, nimwabuduye kwa dhamiri safi tangu zamani za wazee yangu, kama vile nikukumbukavyo wewe daima, katika kuomba kwangu usiku na mchana. (4) Nami natamani sana kukuona, nikiyakumbuka machozi yako, ili nijae furaha; (5) nikiikumbuka imani uliyo nayo isiyo na unafiki, ambayo ilikaa kwanza katika bibi yako Loisi, na katika mama yako Eunike, nami nasadiki wewe nawe unayo. (6) Kwa sababu hiyo nakukumbusha, uichocheee karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu. (7) Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi.

(8) Basi usiuonee haya ushuhuda wa Bwana wetu, wala usinionee haya mimi mfunywa wake, bali uvumilie mabaya pamoja na nami kwa ajili ya Injili, kwa kadiri ya nguvu ya Mungu; (9) ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele, (10) na sasa inadhihirishwa kwa kufunuliwa kwake Mwokozi wetu Kristo Yesu; aliyebatili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili; (11) ambayo kwa ajili ya hiyo naliwekwa niwe mhubiri na mtume na mwali-mu. (12) Kwa sababu hiyo nimepatikana na mateso haya, wala sitahayari; kwa maana namjua yeye niliyemwamini, na kusadiki ya kwamba aweza kukilinda kile nilichokiweka amana kwake hata siku ile. (13) Shika kielelezo cha maneno yenye uzima uliyoyasikia kwangu, katika imani na

KIJANA ALIYEPENDA KITABU CHA MUNGU

upendo ulio katika Kristo Yesu. (14)
Ilinde ile amana nzuri kwa Roho Mtakatifu
akaaye ndani yetu.

SHERIA YA MUNGU KWA MWILI WETU

MASOMO YA BIBLIA: Danieli 1:1-15,17, 20

Ikiwa unajaribu kwenda mahali fulani ambapo hupajui, utamwuliza mtu mwingine kukuonyesha njia. Labda unaweza kumwomba mtu huyo kukuongoza.

Wakati mwingine tunakuwa na shida kufanya uchaguo unaofaa maishani mwetu. Biblia inaweza kutuongoza katika uchaguo wote tunaoweza kufanya. Mungu anajali kila sehemu ya maisha yetu. Hebu tuone jinsi Mungu alivyomwongoza Danieli kufanya uchaguo wa haki jüu ya chakula. Mungu anajali miili yetu.

Danieli alikuwa mbali sana na nyumbani kwao Yerusalemu. Alikuwa mfungwa wa Nebukadreza mfalme wa Babeli. Vijana wengine wengi kutoka Yuda pia walikuwa wafungwa.

Mfalme Nebukadreza alimwambia afisa wake mkuu kuwachagua vijana wenye nguvu kati ya Wayahudi wale wafungwa. Alitaka vijana hao kufundishwa kumtumikia katika makao yake ya mfalme wa Babeli. Aliamuru wafundishwe lugha ya Wababeli, Pia, alitaka wajue historia ya watu wake.

Vijana ambao wangechaguliwa wangepundishwa kwa miaka mitatu. Wakati huu wangelishwa chakula chema cha mfalme na divai ambayo mfalme alikunywa.

Danieli, Shadraka, Meshaki na Abednego walikuwa vijana wanne kati ya vijana waliochaguliwa kumtumikia mfalme. Danieli alisikia kwamba wangelishwa chakula cha mfalme na kunyweshwa divai ya mfalme. Alifikiria jambo ambalo angefanya. Alijua kwamba sheria za Mungu hazikuwaruhusu Wayahudi kula chakula kama kile ambacho Nebukadreza alikula.

Danieli alikata shauri Moyoni mwake kwamba hangekula chakula cha mfalme wala hangekunywa divai yake. Alijua kwamba chakula cha mfalme hakingeweza kufanya



mwili wake kuwa na nguvu. Divai ya mfalme ingemfanya asiweze kufikiri na kutenda mambo kwa njia nzuri.

Danieli alizungumza na afisa ambaye angewalisha. Alimwomba kumruhusu kula chakula tofauti na kile cha mfalme.

Mungu alimfanya afisa yule kumpenda Danieli katika njia maalum. Lakini alio-gopa dokezo lake.

Alimwambia Danieli, "Mimi namwogopa bwana wangu, mflame, aliyewaagizia ninyi chakula chenu na kinywaji chenu; kwa nini azione nyuso zenu kuwa hazipendezi kama nyuso za vijana hirimu zenu? Basi kwa kufanya hivyo mtahatarisha kichwa changu mbele ya mfalme." (Danieli 1:10)

Danieli alimwomba afisa yule kuwaruhusu kula mboga na kunywa maji kwa muda wa siku kumi. Katika mwisho wa siku hizo kumi afisa angewalinganisha na vijana wengine waliokula chakula cha mfalme na kunywa divai ya mfalme. Kisha angekata shauri kama Danieli na marafiki zake wangeendelea kula mboga na kunywa maji. Afisa alikubali kuwaruhusu Danieli, Shadraka, Meshaki, na Abednego kula mboga na kunywa maji kama walivyotaka.

Hata mwisho wa siku zile kumi, afisa yule aliwatazama Danieli na marafiki zake. Bila shaka alishangaa! Vijana hawa walionekana kuwa na nguvu zaidi kuliko vijana wengine waliokula chakula cha mfalme na kunywa divai ya mfalme. Aliwaruhusu kuendelea kula kama walivyotaka.

Mungu aliwabariki Danieli na marafiki zake. Aliwasaidia kuwa na nguvu zaidi na kuwa na hekima. Baada ya vijana wote kufundishwa kwa miaka mitatu, afisa aliwapeleka mbele ya mfalme Nebukadreza. Kati ya vijana hao wote waliochaguliwa kuwa watumishi wa mfalme, hakuna kijana hata mmoja aliyekuwa na nguvu nyingi na hekima kama Danieli na marafiki zake.

Kuna kifungu katika Agano Jipya kitakachotuongoza kutunza miili yetu.

"Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu kati-ka miili yenu." (1 Wakorintho 6:19, 20)

Kifungu hiki kinasema kwamba ukiwa Mkristo, mwili wako ni hekalu ambalo Roho Mtakatifu anakaa. Kwa hivyo tunza mwili wako. Usile wala usinywe kitu chochote kitakachodhuru au kitakachofanya mwili wako kuwa dhaifu.

Tumbaku inaweza kuleta ugonjwa wa "cancer" katika mapafu yako. Pombe inakufanya kutenda mambo kama mpumbavu. Huwezi kutembea vizuri. Huwezi kufikiri vizuri. Watoto wanakosa kupata chakula cha kuto-sha au nguo kwa sababu baba au mama yao anatumia pesa zote kununulia pombe.

Vifungu hivi katika 1 Wakorintho vinatwambia kwamba sisi si mali yetu wenyewe. Hatuwezi kufanya mambo tunayo-

taka kufanya ili kujipendeza wenyewe. Ni lazima tule chakula kitakachofanya miili yetu kuwa na nguvu na afya. Ni lazima tufanye miili yetu kuwa safi. Ni lazima tufanye mambo yanayompendeza Bwana wetu Yesu Kristo.

Usisahau amri za Mungu kuhusu kufanya miili yetu kuwa na nguvu. Mwombe Mungu akusaidie kufanya mambo yale tu yatakayompendeza na kumtukuza.

KAZI YA KUFANYA:

Katika somo hili letu la leo tumeji-funza juu ya kijana mmoja shujaa aliye-itwa Danieli. Alikuwa mtiifu na alifuata amri za Mungu juu ya kula chakula kinachofaa. Tazama kama unaweza kukumbuka juu ya hadithi hiyo.

Hapa kuna maswali ya kukujaribu. Chini ya maswali haya kuna maneno. Chagua neno litakalojibu kila swali sawasawa.

1. Danieli alikuwa mfungwa katika nchi ya _____.
2. Mfalme wa nchi hiyo aliitwa _____.
3. Mfalme aliwachagua vijana wengine _____ katika makao yake ya mfalme.
4. Marafiki watatu wa Danieli waliochaguliwa waliitwa _____, _____ na _____.

SHERIA YA MUNGU KWA MWILI WETU

5. Danieli na marafiki zake walikataa kula _____ cha mfalme na kunywa _____ yake.
6. Danieli na marafiki zake walikula _____ na walikunywa _____.
7. Danieli na marafiki zake walifundishwa kwa muda wa miaka _____.
8. Wakati mafunzo yao yalipomalizika, hakuna kijana hata mmoja aliyekuwa na _____ na _____ kama Danieli na marafiki zake.

(Hapa kuna maneno ambayo ni majibu ya maswali hayo: mboga, nguvu, Babeli, kufundishwa, Meshaki, chakula, Abednego, Nebukadreza, mitatu, hekima, Shadraka, maji, divai).

Tazama kama unaweza kujaza mistari katika kifungu kinachofuata. Kifungu hiki kinatuonyesha sababu inayotupasa sisi kutunza miili yetu.

"Au hamjui ya kuwa _____ wenu ni _____ la _____ aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana _____ kwa _____.

Sasa basi, mtukuzeni _____ katika _____ yenu."

1 Wakorintho 6:19, 20)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Mikono yako ilinifanya ikanitenge-
neza, unifahamishe nikajifunze
maagizo yako." Zaburi 119:73

Ndiyo, Mungu ametuuumba. Ametupa amri zake. Kifungu hiki kinaonyesha kwamba tunaweza kumwomba Mungu kutupa ufahamu ili tuweze kujifunza amri zake. Mwombe Mungu kukusaidia kufahamu neno lake. Atajibu maombi yako. Soma Yakobo 1:5.

MANENO YA KUJIFUNZA:

hirimu.....umri, wenye umri mmoja husema kuwa hirimu moja.
divai.....kinywaji kilichofanywa kwa maji ya zabibu au matunda mengineyo

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Danieli 1:1-15, 17, 20

Katika mwaka wa tatu wa kumiliki kwake Yehoyakimu, mfalme wa Yuda, Nebukadrez,* mfalme wa Babeli, alikwenda Yerusalemu akamshukuru. (2) Bwana akamtia Yehoyakimu, mfalme wa Yuda, katika mkono wake, pamoja na baadhi ya vyombo vya nyumba ya Mungu; naye akavichukua mpaka nchi ya Shinari, mpaka nyumba ya mungu wake; akaviingiza vile vyombo katika nyumba ya hazina ya mungu wake. (3) Mfalme akamwambia Ashpenazi, mkuu wa matowashi wake, awalete baadhi ya wana wa Israeli, wa uzao wa kifalme, na wa uzao wa kiungwana; (4) vijana wasio na mawaa, wazuri wa uso, wajuzi wa hekima, werevu kwa sababu ya maarifa yao, wenye kufahamu elimu, watakaoweza kusimama katika jumba la mfalme; tena alimwambia awafundishe elimu ya Wakaldayo, na lugha yao. (5) Huyu mfalme akawaagizia posho ya chakula

cha mfalme, na ya divai aliyokunywa, aka-agiza walishwe hivyo muda wa miaka mitatu; ili kwamba hatimaye wasimame mbeye ya mfalme.

(6) Basi katika hao walikuwapo baadhi ya wana wa Yuda, Danieli, na Hanania, na Mishaeli, na Azaria. (7) Mkuu wa matowashi akawapa majina; alimwita Danieli Belteshaza; na Hanania akamwita Shadraka; na Mishaeli akamwita Meshaki; na Azaria akamwita Abednego. (8) Lakini Danieli aliazimu moyoni mwake ya kuwa hatajtia unajisi kwa chakula cha mfalme, wala kwa divai aliyokunywa; basi akamwomba yule mkuu wa matowashi ampe ruhusa asijitie unajisi. (9) Basi Mungu alimjalia Danieli kupata kibali na huruma machoni pa huyo mkuu wa matowashi. (10) Mkuu wa matowashi akamwambia Danieli, Mimi namwogopa bwana wangu, mfalme, aliyewaagizia ninyi chakula chenu na kinywaji chenu; kwa nini azione nyuso zenu kuwa hazipendezi kama nyuso za vijana hirimu zenu? basi kwa kufanya hivyo mtahatirisha kichwa changu mbele ya mfalme. (11) Ndipo Danieli akamwambia yule msimamizi, ambaye mkuu wa matowashi amemweka juu ya Danieli, na Hanania, na Mishaeli, na Azaria, (12) Tafadhali utujaribu sisi watumishi wako muda wa siku kumi; na watupe mtama tule, na maji tunywe. (13) Kisha nyuso zetu zitazamwe mbele yako, na nyuso za wale vijana wanaokula chakula cha mfalme; ukatutendee sisi watumishi wako kadiri ya utakavyoona. (14) Basi akawasikiliza katika jambo hilo, akawajaribu siku kumi. (15) Hata mwisho wa zile siku kumi nyuso zao zilikuwa nzuri zaidi, na miili yao

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

ilikuwa imenenepa zaidi, kuliko wale vijana wote waliokula chakula cha mfalme.

(17) Basi, kwa habari za hao vijana wanne, Mungu aliwapa maarifa na ujuzi katika elimu na hekima; Danieli naye alikuwa na ufahamu katika maono yote, na ndoto. (20) Na katika kila jambo la hekima na ufahamu alilowauliza mfalme, akawaona kuwa walifaa mara kumi zaidi ya waganga na wachawi waliokuwa katika ufalme wake.

JINSI YESU ALIVYOTUMIA BIBLIA

MASOMO YA BIBLIA: Mathayo 4:1-11

Je! unajua vifungu vingapi vya Biblia kwa moyo? Labda mwalimu wenu atawapa mashindano darasani asubuhi ya leo. Tazama kwamba ni nani anayeweza kusema vifungu vingi kwa moyo.



Yesu alianza kujifunza Neno la Mungu wakati alipo-kuwa kijana mdogo. Ilikuwa desturi yake kwenda sinagogini kila wiki. Alisikiliza kwa makini wakati waalimu waliposoma maandiko katika hati ya kuviringisha. Mama yake na Yusufu pia walimfundisha nyumbani. Ali-

penda Neno la Mungu na alisema vifungu vingi kwa moyo.

Je! unakumbuka wakati Yesu pamoja na mama yake na Yusufu walipokwenda hekaluni? Alijibu maswali yote aliyoulizwa na waalimu. Yeye pia aliwauliza waalimu maswali! Wakati huo alikuwa na umri wa

miaka kumi na miwili tu.

Wakati wa Yesu kuanza kazi yake ulipofika, alikwenda kwa Mto wa Yordani. Yohana Mbatizaji alikuwa akihubiri na kuwabatiza watu pale. Alimbatiza Yesu.

Baada ya Yesu kubatizwa, aliongozwa na Roho nyikani. Alijaribiwa na Ibilisi huko. Alikaa huko siku arobaini mchana na usiku bila kula chakula. Mwisho wake aliona njaa.

Kisha Ibilisi alimjia Yesu, aka-mwambia, "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate." (Mathayo 4:3)

Yesu alikumbuka kifungu alichojifunza katika Neno la Mungu kilichosema: "...mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha Bwana." (Kumbukumbu la Torati 8:3) Yesu alikataa kutumia uwezo wake kuridhisha njaa yake. Alimwamini Mungu kumpa chakula.

Ibilisi alimchukua Yesu mpaka mji mtakatifu. Alimweka juu ya kinara cha hekalu. Alimwambia, "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini; kwa maana imea-ndikwa, Atakuagizia malaika zake; Na mikononi mwao watakuchukua; Usije ukaji-



kwaa mguu wako katika jiwe." (Mathayo 4:6)

Ibilisi alipokwisha kusema maneno haya, Yesu alikumbuka kifungu kingine kilichosema: "Msimjaribu Bwana, Mungu wenu...." (Kumbukumbu la Torati 6:16) Yesu alijua kwamba haikuwa haki kwake kujiingiza hatarini kisha kumtumainia Mungu kumlinda.

Ibilisi alimjaribu Yesu mara ya tatu. Alimchukua Yesu mpaka mlima mrefu mno. Alimwonyesha milki zote za ulimwengu. Alisema, "Haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia." (Mathayo 4:9)

Kisha Yesu alimwambia Ibilisi kuondoka kwake! Alisema, "Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake." (Mathayo 4:10)

Kwa sababu Yesu alijua Neno la Mungu, alijua jinsi ya kumjibu Ibilisi wakati alipomjaribu. Shetani hushindwa kwa Neno la Mungu! Ikiwa unajua mambo Mungu anayotaka, wewe pia unaweza kumwambia Ibilisi kuondoka kwako. Neno la Mungu linakufundisha amri zake. Ukijua amri hizi unaweza kuwa mtiifu.

Wakati unapojaribiwa na Shetani kuchukua, ukumbuke kwamba Yesu alisema, "...Wapendeni adui zenu...." (Mathayo 5:44) Kwa hivyo unaweza kumwambia Shetani, "Ondoka kwangu Shetani kwa sababu Neno la Mungu linasema, 'Wapendeni adui zenu.'"

Wakati fikira mbaya zinapokuja aki-
lini mwako, umwambie
Shetani mara moja
kuondoka kwako. Umwa-
mbie kwamba Mungu
anasema katika Bib-
lia, "Hatimaye,
ndugu zangu mambo
yo yote yaliyo ya
kweli, yo yote
yaliyo ya staha, yo
yote yaliyo ya haki,
yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye
sifa njema... yatafakarini hayo." (Wafi-
lipi 4:8) Ukitumia Neno la Mungu katika
njia hii, Shetani atakuacha. Umjibu
haraka kwa Neno la Mungu na ataondoka
kwako.



Wakati wa wiki ijayo ujaribu kutu-
mia Neno la Mungu kila wakati unapojari-
biwa. Wakati unapokuja kwa Shule ya Juma-
pili, uwaambie mwalimu na rafiki yako
jinsi Mungu amekusaidia.

KAZI YA KUFANYA:

Somo hili letu limeonyesha njia
ambazo Yesu alitumia Neno la Mungu. Yeye
ndiye mfano wetu. Mungu ametupa Neno
lake kutuongoza. Ni lazima tujue Neno la
Mungu na kulitumia kama Yesu alivyolitu-
mia.

Jibu maswali yafuatayo hapo chini.
Utaona kama umekumbuka kiasi gani njia
ambazo Yesu alitumia Neno la Mungu. Kuli-

kuwa na mifano mingine juu ya Neno la Mungu kuhusu kumshinda Shetani. Tazama kama unaweza kukumbuka mifano hiyo.

1. Yesu alianza kujifunza Neno la Mungu wakati alipokuwa _____.
2. Ilikuwa _____ yake kwenda _____ kila wiki.
3. Yesu alikuwa na umri wa miaka _____ wakati alipojibu maswali ya waalimu hekaluni.
4. Yesu alibatizwa na _____.
5. Baada ya Yesu kubatizwa, aliongozwa na _____ kwenda nyikani.
6. Alikaa huko siku _____ mchana na usiku.
7. Jaribu la kwanza la Ibilisi lili-
mtaka Yesu kuyaamuru mawe kuwa
_____. Yesu alimjibu Ibilisi kwa
kutumia kifungu cha Kumbukumbu la
Torati 8:3. Tafuta kifungu hicho
katika Biblia yako.

Andika maneno sawasawa katika mista-
ri iliyoachwa:

"...mwanadamu haishi kwa _____ tu,
bali huishi kwa kila litokalo kati-
ka _____ cha _____."
(Kumbukumbu la Torati 8:3)

8. Baada ya jaribu lake la pili, Yesu alimjibu Ibilisi kwa kifungu hiki cha Kumbukumbu la Torati 6:16. Jaza mistari iliyoachwa: "Msimjari-bu Bwana, _____ wenu...."
9. Baada ya jaribu lake la tatu, Yesu alimjibu Ibilisi kwa maneno haya: "Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie _____ wako, umwabudu yeye peke yake." (Mathayo 4:10)
10. Wakati unapojaribiwa kuchukia, ukumbuke kwamba Yesu alisema, _____ adui zenu." (Mathayo 5:44)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutenda dhambi."

Zaburi 119:11

Yesu aliweza kumshinda Shetani kwa kutumia Neno la Mungu kwa sababu aliliweka Neno hilo moyoni mwake. Ni lazima sisi tufanye kama Yesu alivyofanya. Ni lazima tufanye kama tunavyoambiwa na kifungu chetu cha kukumbuka. Jifunze Neno la Mungu kwa moyo. Jitayarishe mwenyewe kumshinda Shetani ukitumia Neno la Mungu.

MANENO YA KUJIFUNZA:

Ibilisi.....Shetani, mshawishi

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mathayo 4:1-11

Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi. (2) Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa. (3) Mjaribu akamjia akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. (4) Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu. (5) Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, (6) akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini; kwa maana imeandikwa, Atakuagizia malaika zake; Na mikononi mwao watakuchukua; Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe. (7) Yesu akamwambia, Tena imeandikwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako. (8) Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake, (9) akamwambia, Haya yote nitakupa, ukianguka kuni-sujudia. (10) Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake. (11) Kisha Ibilisi akamwacha; na tazama, wakaja malaika wakamtumikia.

WATENDAJI WA NENO

MASOMO YA BIBLIA: Mathayo 25:31-46

Je! ukitaka kumwonyesha rafiki yako kwamba unampenda, utamfanyia nini? Utamtendea jambo muhimu zaidi kuliko kumwambia tu kwamba "Ninakupenda," sivyo? Ndiyo, utajaribu kumtendea kitu chema au cha kumsaidia. Kwa kuwa mwema au mwenye kusa- idia, unaonyesha upendo wako hasa kwa rafiki yako. "Tendo" lako linalingana na "msemo" wako.



Katika somo letu la Biblia leo Yesu alikuwa akizungumza juu ya mojawapo ya mambo yatakayofanyika wakati atakapokuja tena. Alisema kwamba ataketi katika kiti chake cha utukufu na malaika wote watakuwa pamoja naye.

Wakati huo mataifa yote watakusanyika mbele za Yesu. Biblia inasema, "... naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi, atawaweka kondoo mkono wake wa kuume, na mbuzi mkono wake wa kushoto." (Mathayo 25:32,33)

Kisha Yesu atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, "Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowe- kewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu." (Mathayo 25:34b)

Je! ni watu gani walioitwa kondoo na kuwekwa mkono wa kuume wa Yesu? Yesu aliwaambia, "kwa maana nalikuwa na njaa,

mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkani-nyweshu; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika; nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifu-ngoni, mkanijia." (Mathayo 25:35, 36)

Watu hao walioko mkono wa kuume wa Yesu watataka kujua wakati walipomfanyia mambo hayo.

Yesu atajibu, "...Amin, nawaambia, kadiri mliyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi." (Mathayo 25:40b)

Hii ni jambo la ajabu sana kufikiria! Yesu alisema kwamba tunapowalisha wenye njaa au tunapowatembelea wagonjwa, haya yote tunamtendea yeye. Anapendezwa sana wakati tunapoonyesha upendo wetu kwa kuwa wema na kuwasaidia watu wengine anaowapenda.

Yesu atawaambia wale walioko mkono wake wa kushoto, "Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake." (Mathayo 25:41b) Watu walioko mkono wake wa kushoto ni wale waliokataa kuwasaidia watu waliokuwa na mahitaji. Yesu alisema ya kwamba, kwa kuwa walikataa kusaidia, walimkataa yeye pia.

Somo hili linaonyesha wazi kwamba ni lazima tuonyeshe upendo wetu kwa mate-ndo yetu kwa wengine. Je! mtu akija nyumbani kwako akisema, "Nina njaa. Tafadhali, nipe chakula nile," utafanya nini?

Utamwambia, "Nasikitika, sina kitu cha kukupa. Natumaini utapata chakula mahali pengine?"

Kusema, "Nasikitika" si kuonyesha upendo kwa mtu yule aliye na njaa. Lakini kumpa chakula ni kuonyesha upendo. Kujua Neno la Mungu peke yake hakutoshi. Ni lazima tufanye mambo linalosema.

Neno la Mungu linasema, "Enyi wato-to, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki." (Waefeso 6:1) Amri hii inatoka kwa Mungu. Ukitaka kutii amri hii ni lazima uwatii wazazi wako. Ni lazima uwe "mtendaji" wa Neno la Mungu na "msikiaji" ili uweze kumpendeza Yesu.

Siku moja Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Mkinipenda, mtazishika amri zangu." (Yohana 14:15) Unapoendelea kukua, utajifunza mengi juu ya amri za Yesu. Je! utamwonyesha Yesu kwamba unampenda kwa kutii amri zake?

Mwombe Mungu kukusaidia kuwa mtendaji wa Neno lake. Kumbuka kwamba kusikia tu Neno la Mungu bila kutenda jambo analosema hakumpendezi.



KAZI YA KUFANYA:

Somo letu la leo linatuonyesha wazi kwamba kujua Neno hakutoshi. Ni lazima pia tufanye mambo linalosema.

Hapo kuna mifano ya wavulana na wasichana waliosikia Neno la Mungu. Walisikia mambo Mungu aliyoamuru. Mwisho wa kila mfano kuna mstari. Ikiwa kijana huyo alifanya mambo ambayo Mungu alisema, uandike "mtendaji" kwenye mstari. Ikiwa hakufanya mambo ambayo Mungu alisema, uandike "msikiaji."

1. Petro alijifunza kifungu chake cha kukumbuka katika Shule ya Jumapili. Kifungu hicho kilisema, "Enyi wato-to, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki." (Waefeso 6:1)

Wiki ya pili yake mamaye Petro alikwenda shambani kulima. Alimwambia Petro kumtunza dada yake mdogo. Petro alikwenda nyumbani mwa jirani yao. Hakumtunza dada yake. Je! Petro alikuwa "msikiaji" au "mtendaji?"

Petro alikuwa _____

2. Mwalimu wa Paulo wa Shule ya Jumapili alisoma kifungu darasani. Kifungu hicho kilisema, "Siku ya hofu yangu nitakutumaini wewe." (Zaburi 56:3)

Paulo aliogopa giza. Aliogopa pepo au mashetani walioko shambani. Aliogopa kulogwa. Je! Paulo alikuwa "msikiaji" au "mtendaji?"

Paulo alikuwa _____.

3. Siku moja asubuhi mchungaji wa akina Mariamu alihubiri juu ya dhambi ya kukasirika. Alisoma kifungu kutoka Mithali. Kifungu hicho kili-sema, "Jawabu la upole hugeuza hasira." (Mithali 15:1)

Siku ya pili yake shuleni Dora, rafikiye Mariamu, alimkasirikia na kumkemea. Mariamu alimkataza Dora kuandika majibu yake wakati wa mtihani. Dora alimkemea sana.

Lakini Mariamu alikumbuka kifungu alichojifunza siku ya Jumapili. Kwa hivyo hakukasirika wakati alipokemewa. Alimwambia Dora kwa upole: "Nasikitika Dora, lakini siwezi kukuruhusu kuandika majibu yangu. Kufanya hivyo ni kudanganya." Je! Mariamu alikuwa "msikiaji" au "mtendaji?"

Mariamu alikuwa _____.

4. Siku moja Simoni alikuwa akisoma Biblia yake. Alisoma kifungu hiki katika Waefeso: "Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi." (Waefeso 4:32)

Simoni alipenda kifungu hicho sana. Alifurahi sana kufikiria kwa-mba Mungu alisamehe dhambi zake. Pia alijua kwamba ilimpasa kuwasamehe wengine wakati walipomkosea.

Siku moja Simoni na Daudi, rafiki yake, walikuwa wakicheza na mpira wake. Daudi aliupiga mpira ule, kisha ukapiga kipande cha chupa kilichovunjika, ukatoboka. Simoni alikasirika sana. Daudi alimwambia, "Simoni, nasikitika. Tafadhali unisamehe. Mpira huo umetoboka kwa ajali tu."

Lakini Simoni alipaza sauti yake kwa hasira, akasema, "Sitakusamehe. Lazima utanilipa." Simoni alichukua mpira wake, akaenda nyumbani. Daudi alihuzunika sana. Je! Simoni alikuwa "msikiaji" au "mtendaji?"

Simoni alikuwa _____.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidana ganya nafsi zenu." Yakobo 1:22

Je! unaona tofauti katika kuwa "msikiaji" wa Neno la Mungu na kuwa "mtendaji" wa Neno hilo? Ni kweli kwamba lazima ulisikie Neno hilo. Hivyo ndivyo unavyojua mambo ambayo Mungu anakutaka wewe kufanya. Lakini ni lazima pia ufanye

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

mambo ambayo Neno hilo linasema. Mwombe
Mungu kukusaidia daima kuwa "mtendaji"

MANENO YA KUJIFUNZA:

kulogwa.....kutiwa uchawi, kumfanyia
mtu uchawi ni kumloga.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mathayo 25:31-46

Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu kati-
ka utukufu wake, na malaika watakatifu
wote pamoja naye, ndipo atakapoketi kati-
ka kiti cha utukufu wake; (32) na mataifa
yote watakusanyika mbele zake; naye atawa-
bagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo
na mbuzi; (33) atawaweka kondoo mkono
wake wa kuume, na mbuzi mkono wake wa
kushoto. (34) Kisha Mfalme atawaambia
wale walioko mkono wake wa kuume, Njoni,
mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufa-
lme mliowekewa tayari tangu kuumbwa uli-
mwengu; (35) kwa maana nalikuwa na njaa,
mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkan-
nywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha;
(36) nalikuwa uchi, mkanivika; nalikuwa
mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifu-
ngoni, mkanijia. (37) Ndipo wenye haki
watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini
tulipokuona una njaa, tukakulisha, au
una kiu tukakunywesha? (38) Tena ni lini
tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au
u uchi, tukakuvika? (39) ni lini tena
tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni,
tukakujia? (40) Na Mfalme atajibu, akiwa-
ambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomte-

ndea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi. (41) Kisha ata-waambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake; (42) kwa maana nalikuwa na njaa, msinipe chakula; nalikuwa na kiu, msininyweshe; (43) nali-kuwa mgeni, msinikaribishe; nalikuwa uchi, msinivike; nalikuwa mgonjwa, na kifungoni, msije kunitazama. (44) Ndipo hao pia watajibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona wewe una njaa, au una kiu, au u mgeni, au u uchi, au u mgonjwa, au u kifungoni, tusikuhudumie? (45) Naye atawajibu, akisema, Amin, nawaambia, Kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea mimi. (46) Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele.

WAKATI MUNGU ALIPOTOA SHERIA ZAKE

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20;1-17

Wana wa Israeli walikuwa njiani kwenenda Nchi ya Ahadi. Walikuwa jangwani mbele ya Mlima wa Sinai.

Walipokuwa jangwani, wana wa Israeli walinung'unika kila siku. Musa alishindwa kuleta amani kati yao. Hata mara nyingi alimwomba Mungu kumsaidia. Sasa wana wa Israeli walifika chini ya Mlima wa Sinai wakiwa bado wakigombana na kunung'unika.

Musa alipanda Mlima wa Sinai kusema na Mungu. Mungu alimwambia kuwakumbusha wana wa Israeli juu ya ulinzi wake kwa kuwatoa katika nchi ya Misri. Alimwambia Musa kuwaambia kukumbuka jinsi alivyowapa chakula na maji jangwani.

Kisha Mungu alimwambia Musa kuwaambia wana wa Israeli kwamba alitaka kusema nao. Alimwambia Musa kuwaambia kuwa tayari.

Musa alishuka mlimani, akawaambia wana wa Israeli mambo yote ambayo Mungu alimwambia. Aliwaambia kujitayarisha. Walifua nguo zao, wakafanya mambo yote ambayo Mungu aliwaambia kufanya. Walitaka kuwa tayari kumsikiliza Mungu.

Siku ya tatu wakati wa asubuhi, watu walisikia ngurumo na umeme. Walipotazama, waliona wingu zito juu ya mlima. Mara walisikia sauti ya baragumu iliyolia sana.

Watu wote walimfuata Musa mara moja kuto-ka kambini mwao kwenda Mlima wa Sinai. Wote walifika, wakasimama pande za chini za mlima. Walitazama wakati moshi ulipokuwa ukitoka katika mlima kama moshi wa tanuru. Mlima wote ulitetemeka sana.



Mungu alisema na wana wa Israeli, akawaambia, "Mimi ni Bwana, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa." (Kutoka 20:2)

Kisha Mungu aliwapa sheria zake kumi. Sheria hizi zinaitwa Amri Kumi za Mungu. Mungu alisema ya kwamba Waisraeli wangukuwa watu wake maalum kama wangemtii. Alikuwa na mpango kuubariki ulimwengu wote kwa taifa la Waisraeli. Lakini alisema ilikuwa lazima kwa Waisraeli kutii amri zake na kumwabudu yeye peke yake.

Hizi ndizo sheria kumi za Mungu zinazojulikana kama Amri Kumi za Mungu.

1. Usiwe na miungu mingine ila mimi.
(kifungu cha 3)
2. Usijifanyie sanamu ya kuchonga....
(kifungu cha 3)

3. Usilitaje bure jina la Bwana,
Mungu wako.... (kifungu cha 7)
4. Ikumbuke siku ya sabato uitakase.
(kifungu cha 8)
5. Waheshimu baba yake na mama yako.
(kifungu cha 12)
6. Usiue....(kifungu cha 13)
7. Usizini....(kifungu cha 14)
8. Usiibe....(kifungu cha 15)
9. Usimshuhudie jirani yako uongo....
(kifungu cha 16)
10. Usitamani....(kifungu cha 17)

Wana wa Israeli walingojea chini ya mlima. Musa alipanda juu, akaingia katika wingu zito ambamo Mungu alikuwamo. Kisha Mungu alimwambia mambo mengi juu ya sheria zake.

Halafu Musa alishuka mlimani. Aliwambia watu mambo ambayo Mungu alitaka wafanye. Watu hao walisema kwa moyo hasa, "Hayo yote aliyoyanena Bwana tutayatenda, nasi tutatii." (Kutoka 24:7)

Kwa kuwa sheria hizi ni muhimu zana, itakuwa vyema kwako kujifunza. Je! utajaribu kwa msaada wa Mungu kutovunja hata mojawapo ya sheria hizo?

Kumbuka kwamba Yesu alisema tukimpenda, tutatii amri zake. Mwombe kukusaidia kuwa kijana mtiifu wa Mungu, anayesema, "Hayo yote aliyoyanena Bwana tutayatenda, nasi tutatii." (Kutoka 24:7)

WAKATI MUNGU ALIPOTOA SHERIA ZAKE

Ikiwa hujui Amri Kumi za Mungu, je! utajaribu kujifunza kabla Jumapili ijayo? Wakati unapokuja kwa Shule ya Jumapili, unaweza kuzisema kwa mwalimu wako.

KAZI YA KUFANYA:

Umesikia katika somo lako leo juu ya wakati ambapo Mungu aliposema na wana wa Israeli. Walikuwa wakisafiri jangwani. Walikwisha kufika katika Mlima wa Sinai.

Hapo chini kuna kukujaribu kuona mambo unayokumbuka juu ya hadithi hii. Andika majibu katika mistari.

1. Musa alipanda Mlima wa Sinai kusema na _____.
2. Mungu alimwambia Musa kuwaambia wana wa Israeli kukumbuka kwamba aliwapa _____ na _____ jangwani.
3. Mungu alimwambia Musa kuwaambia wana wa Israeli kuwa tayari kwa sababu alitaka _____ nao.
4. Wana wa Israeli walisikia _____ na _____ mlimani.
5. Walisikia sauti ya _____ ili-yolia sana.
6. Mungu alisema na wana wa Israeli, akawaambia, "Mimi ni Bwana, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya _____." (Kutoka 20:2)

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

7. Sheria kumi ambazo Mungu alimpa Musa zinaitwa _____.
8. Mungu alisema Waisraeli wangekuwa watu wake _____.
9. Mungu alisema iliwapasa watu kuwa _____ kwa sheria zake na kumwa-
budu yeye _____ yake.
10. Wakati Musa alipowaambia wana wa Israeli mambo Mungu aliyosema kwa-
mba iliwapasa kufanya, walimjibu,
" _____ aliyoyanena
Bwana _____, nasi _____."
(Kutoka 24:7)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

*"Kisha akakitwaa kitabu cha agano akakisoma masikioni mwa watu; wakase-
ma, Hayo yote aliyoyanena Bwana tuta-
yatenda, nasi tutatii." Kutoka 24:7*

Wana wa Israeli walisikia mambo ambayo Mungu alisema kwamba iliwapasa kufanya. Tunaona majibu yao katika kifungu cha kukumbuka. Je! walisema nini? Ndiyo, walisema watafanya mambo yote Mungu aliyoyasema.

Wana wa Israeli, sikuzote hawakufanya mambo Mungu aliyoyasema. Walitenda dhambi mara nyingi. Lakini wakati walipomrudia Mungu kumwomba msamaha, Mungu aliwasamehe.

Sikuzote hutafanya mambo Mungu anayosema. Je! utafanya nini wakati utakapomtenda Mungu dhambi? Mungu ana ahadi kwako katika Neno lake, "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." (1 Yohana 1:9)

Hii ni ahadi ya ajabu kutoka kwa Baba yetu aliye mbinguni. Je! anawambia kufanya nini wakati tunapotenda dhambi? Anawambia kutubu dhambi zetu. Je! utafanya mambo anayosema? Utaungama dhambi zako kila siku?

Katika somo la tano, kifungu chetu cha kukumbuka kinawambia mambo yanayotupasa kufanya ili tusiweze kumtenda Mungu dhambi tena. Je! bado unakumbuka kifungu kile? Ikiwa hukumbuki, ukitafute na kuki-soma tena. Wiki ijayo ujaribu sana kusema Amri Kumi za Mungu kwa moyo. Kuwa tayari kuzisema amri hizo kwa mwalimu wako mta-kapokutana tena.

MANENO YA KUJIFUNZA:

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Kutoka 20:1-17

Mungu akanena maneno haya yote akasema, (2) Mimi ni BWANA, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa. (3) Usiwe na miungu

mingine ila mimi.

(4) Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. (5) Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, (6) nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.

(7) Usilitaje bure jina la BWANA Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.

(8) Ikumbuke siku ya sabato uitakase. (9) Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; (10) lakini siku ya saba ni sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. (11) Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya sabato akaitakasa.

(12) Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako. (13) Usiue. (14) Usizini. (15) Usiibe. (16) Usimshuhudie jirani yako uongo. (17) Usitamani nyumba ya jirani wako, usitamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alichonacho jirani yako.

KUISHI KWA SHERIA ZA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:1-17

Je! ulijifunza Amri Kumi za Mungu kwa moyo wiki iliyopita? Ikiwa ulijifunza, basi umeliweka Neno la Mungu moyoni mwako ili hutaweza kumtenda dhambi.

Neno la Mungu litatusaidia kila siku. Kumbuka kwamba inatupasa kutumia Neno hilo katika vita vyetu na Shetani. Shetani hawezi kushindana na Neno la Mungu.

Mungu aliwapa watu wake sheria zake zamani sana. Sheria hizo za Mungu, mpaka sasa ni muhimu sana. Hebu tujifunze kila mojawapo ya Amri hizo Kumi leo. Tutaona jinsi zinavyoweza kutusaidia kila siku.

1. "Usiwe na miungu mengine ila mimi." (kifungu cha 3)

Katika amri hii tunaambiwa kwamba ni lazima tumpende Mungu zaidi kuliko mtu ye yote au kitu cho chote. Tukipenda kitu cho chote zaidi kuliko kumpenda Mungu, basi kitu hicho kinakuwa mungu wetu. Tuna-kiabudu na kukitumikia badala ya Mungu.

2. "Usijifanyie sanamu ya kuchonga. (kifungu cha 4)

Watu wengi ulimwenguni wanaabudu sanamu za dhahabu na fedha. Watu wengine wanatengeneza sanamu za miti au mawe. Watu wengine wanaofanya hivyo, hawajasikia kamwe habari za Mungu mmoja wa kweli.

Wengine ambao hawajui habari za Mungu na Yesu, ambaye ni Mwokozi, wanatumia sanamu na picha. Wanafikiri kwamba sanamu hizi zitawasaidia kuabudu. Hata wanaabudu sanamu hizi. Mungu anatukataza kutumia sanamu. Sisis sote tunapaswa kumwabudu yeye peke yake.

3. "Usilitaje bure jina la Bwana, Mungu wako...." (kifungu cha 7)

Wakati tunapotaja jina la Mungu, inatupasa kulitaja kwa heshima. Ni lazima tukumbuke kwamba ni jina takatifu. Tunamkasirisha Mungu sana wakati tunapotumia jina lake ovyo bila kujali.

Wakati mwingine watu husema, "haki ya Mungu" wanapotaka wengine kuamini mambo wanayosema. Hii ni njia mbaya ya kutumia jina la Mungu. Wakati mtu anapopapa hivyo, anavunja amri ya tatu ya Mungu. Inatupasa kuwa waangalifu sana kutumia jina la Mungu katika njia ya heshima.

4. "Ikumbuke siku ya sabato uitakase." (kifungu cha 8)

Kutoka wakati Yesu alipofufuka kaburini siku ya kwanza ya juma, siku ya Jumapili imefanywa kuwa siku yetu ya sabato. Tukitii amri hii, hatutafanya mambo mengi tunayofanya kila siku.

Inatupasa kutumia wakati mwingi kupumzika siku hii. Inatupasa kwenda kanisani kumwabudu Mungu. Pia, tunaweza kutafuta

njia za kuwatendea watu wengine mambo mema.

5. "Waheshimu baba yako na mama yako...." (kifungu cha 12)

Mungu anasema kwamba inatupasa kuwaheshimu na kuwatii wazazi wetu. Inatupasa kufanya upesi mambo wanayotwambia. Inatupasa kufanya upesi mambo wanayotwambia. Inatupasa kufanya mambo tunayojua kwamba wanataka tufanye bila kuambiwa. Inatupasa kufanya mambo yanayowapendeza hata wakati ambapo tuko mbali nao.

6. "Usiue." (kifungu cha 13)

Hakuna hata mmoja wetu ambaye angefikiria kumwua mtu. Lakini kuna njia nyingine ya kuvunja amri hii. Tukikasirika sana na mtu na kumtakia mauti, tumevunja amri hii. Mungu anajua mawazo ya moyo yetu.

7. "Usizini." (kifungu cha 14)

Amri hii huvunjwa wakati mume anapoacha mkewe na kuzini na mwanamke mwingine. Huvunjwa wakati mwanamke anapoacha mumewe na kukaa na mume mwingine.

Pia, huvunjwa wakati mume na mke wanapokaa pamoja bila ndoa. Mungu alitupa amri hii kutusaidia kuwa na nyumba nzuri sasa na wakati tutakapokuwa wakubwa.

Njia nzuri ya kutii amri hii sasa ni kufikiria miili yetu kama kipawa kutokea kwa Mungu na kuiweka safi na yenye

afya. Fikira, maneno, na matendo yetu yote ni lazima kuwa safi. Mungu atatusaidia kufanya hivyo wakati tunapomwomba.

8. "Usiibe." (kifungu cha 15)

Maana ya amri hii ni kwamba haitupasi kuchukua kitu cha mtu mwingine. Tuki-chukua kwa makosa au kwa kusudi, ni lazima tukirudishe, au kukilipia.

9. "Usimshuhudie jirani yako uongo."
(kifungu cha 16)

Tusiseme uwongo juu ya watu wengine. Ni lazima tuwe waangalifu sana katika msemu wetu. Tusiwafanye watu wengine kumfikiria mtu mwingine mambo mabaya kwa sababu ya uwongo wetu.

10. "Usitamani...." (kifungu cha 17)

Neno "kutamani" maana yake kushika yote au kuwa mchoyo. Kutamani vitu kuna-weza kuwa tamaa kubwa maishani mwa mtu hata kuchukua nafasi ya Mungu.

Watu wameua, wameiba, wameuza miili yao, wamekataa mashauri ya wazazi kwa sababu ya kutamani. Dhambi hii ni mbaya sana.

Tusitake kitu cha mtu mwingine. Ni dhambi kutaka kuwa na kitu kama cha mtu mwingine. Tunavunja amri hii wakati tunapochukua kitu cha mtu mwingine na kumwachacha bila cho chote.

KUISHI KWA SHERIA ZA MUNGU

Yesu atatusaidia kutii amri hizi. Alijaribiwa mara nyingi lakini hakuvunja amri hata moja. Anajua njia zote tunazojaribiwa. Kwa hivyo anaweza kutusaidia kuwa watiifu na kushika amri za Mungu. Wakati mwingine tutashindwa kwa sababu hatuna nguvu nyingi kama Yesu alivyokuwa nayo. Lakini atatusamehe na atatusaidia kuwa watiifu.

KAZI YA KUFANYA:

Ikiwa hujui Amri zote Kumi kwa moyo, utumie wakati wako wa "Kazi ya Kufanya" kumaliza kujifunza zote.

Hapo chini kuwa picha. Tazama picha hizo kwa uangalifu. Soma maandiko yaliyo chini ya kila picha. Kisha uandike mojawapo ya Amri Kumi za Mungu katika mistari iliyo chini ya kila picha. Vifungu hivyo utakavyosema vitakusaidia kuchagua amri sawa kuandika katika mstari.




Mathayo 26:74,75



Hesabu 15:32-36



1 Samweli 18:6-11



Yohana 12:1-6



Yoshua 7:19-21



Kutoka 32:1-4

KUISHI KWA SHERIA ZA MUNGU

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Sheria ya Bwana ni kamilifu, huiburudisha nafsi. Ushuhuda wa Bwana ni amini humtia mjinga hekima."
Zaburi 19:7

Sheria ya Bwana ni kamilifu. Ni kweli. Haitabadilika kamwe. Haitapita. Hututia nguvu tukijifunza. Itatuongoza tuna-poifuata.

Biblia inasema, "Yeye aishikaye sheria ni mwana mwenye hekima...." (Mithali 28:7). Ukitaka kuwa na hekima ni lazima ujue na kutii Neno la Mungu.

Mwombe Bwana kukusaidia kulipenda kweli Neno lake. Mwombe kukusaidia kuli-fahamu wakati unapoisoma.

MANENO YA KUJIFUNZA:

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Kutoka 20:1-17

Mungu akanena maneno haya yote akasema, (2) Mimi ni BWANA, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa. (3) Usiwe na miungu mingine ila mimi.

(4) Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani,

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

wala kilicho majini chini ya dunia. (5) Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, (6) nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.

(7) Usilitaje bure jila la BWANA Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.

(8) Ikumbuke siku ya sabato uitakase. (9) Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; (10) lakini siku ya saba ni sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. (11) Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya sabato akaitakasa.

(12) Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako. (13) Usiue. (14) Usizini. (15) Usiibe. (16) Usimshuhudie jirani yako uongo. (17) Usiitamani nyumba ya jirani wako, usiitamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alichochacho jirani yako.

YESU AELEZA SHERIA ZA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Marko 12:28-34

Siku moja Yesu alikuwa ndani ya hekalu akiwafundisha watu habari za Mungu. Pia, alikuwa akijibu maswali ya watu hao. Kulikuwa na mwandishi mmoja kati ya watu hao ambao walikuwa wakimsikiliza Yesu. Mwandishi huyu alijitokeza mbele, akamwuliza Yesu swali hili: "Katika amri zote ni ipi iliyo ya kwanza?" (Marko 12:28b)



Labda unaweza kujua jibu ambalo Yesu alimpa mwandishi huyu. Ikiwa huwezi kukumbuka jibu hilo, basi ndilo hili: "Ya kwanza ndiyo hii, Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. Na ya pili ndiyo hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi." (Marko 12:29-31)

Mwandishi yule alipendezwa sana na jibu la Yesu. Alikubali kwamba kumpenda Mungu na kumpenda jirani yetu kama nafsi zetu kunampendeza Mungu zaidi kuliko sadaka za kuteketezwa. Katika Agano la Kale, watu walitoa sadaka za kuteketezwa hekaluni. Lakini Mungu hakupendezwa na

sadaka hizi bila wao wenyewe kumpenda kwa mioyo yao yote.

Yesu alijua mawazo ambayo mwandishi huyu alikuwa nayo moyoni. Alijua kwamba mwandishi huyu alifahamu zaidi upendo wa Mungu kuliko watu wengine. Alimwambia, "...Wewe hu mbali na ufalme wa Mungu...." (Marko 12:34)

Hebu sasa tufikirie zaidi mambo kuhusu amri hizi ambazo Yesu alisema kwamba ndizo kuu. Tumezisoma katika Marko 12:29-31.

Mungu alimpa Musa Amri zake Kumi katika Mlima wa Sinai. Alisema kwamba ilikuwa lazima Waisraeli kuzitii amri hizo ikiwa walitaka kuwa watu wake maalum. Yesu alimwambia mwandishi huyu amri mbili ambazo zilikuwa kuu. Je! alikuwa akimwambia mwandishi amri ambazo zilikuwa tofauti kabisa na Amri Kumi ambazo Mungu alitoa?

Hebu tuangalie Amri Kumi zilizo katika Sura ya Saba ya kitabu hiki. Chora mstari mrefu chini ya amri ya nne. Soma amri nne za kwanza kwa uangalifu.

Halafu sasa soma amri ambayo Yesu alisema kwamba ilikuwa kuu kwa uangalifu Amri hii imeandikwa katika Marko 12:29, 30. Je! ukitii amri hii ambayo Yesu alitoa, unatii pia amri nne za kwanza ambaz Mungu alimpa Musa?

YESU AELEZA SHERIA ZA MUNGU

Ndiyo, unazitii kwa sababu amri hizo nne za kwanza zinaeleza jinsi inavyotupasa kufikiri na kuonyesha matendo yetu kwa Mungu.

Angalia amri sita za mwisho ambazo Mungu alimpa Musa. Sasa soma tena amri ambayo Yesu alitoa kama amri ya pili kuu. Je! ukitii amri hii ya pili ambayo Yesu alitoa, utatii amri sita ambazo Mungu alitoa?

Ndiyo, utakuwa unatii amri hizo kwa sababu amri hizo sita za mwisho zinatwambia jinsi inavyotupasa kufikiri na kuonyesha matendo yetu kwa watu wengine.

Paulo alisema katika Warumi 13:10: "Pendo halimfanyii jirani neno baya; basi pendo ndilo utimilifu wa sheria." Paulo alikuwa akisema ya kwamba upendo ndio utimilifu wa masharti yote ya Mungu.

Je! unampenda Mungu kama Yesu alivyosema kwamba inatupasa kumpenda? Unampenda jirani kama unavyojipenda wewe mwenyewe? Kuwa mwaminifu. Mwombe Mungu kukuonyesha njia ambayo hutii amri zake. Mungu atakusamehe kutotii kwako ikiwa utamwomba.

Mungu anakupenda sana kwa sababu "...Mungu ni upendo." (1 Yohana 4:8) Yesu alisema juu ya upendo kama tunavyosoma katika somo hili letu la leo. Tunapojifunza maisha ya Yesu, tunaona jinsi alivyotenda mambo yake katika upendo. Tunaposoma juu ya kifo chake msalabani

kwa ajili ya dhambi zetu, tunaona alivyo-onyesha upendo wake kwetu.

Yesu alieleza sheria za Mungu wakati alipofundisha. Alionyesha upendo wa Mungu kwa uhai wake.

Mwombe Mungu kukusaidia kuwa na upendo kama anavyotwamuru. Hapa kuna ahadi kutoka kwa Neno kutusaidia: "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu." (Wafilipi 4:13)

KAZI YA KUFANYA:

Umesikia katika somo hili lako leo juu ya wakati ambapo Yesu alikuwa akifundisha hekaluni. Pia, alikuwa akijibu maswali. Alikuwa akieleza baadhi ya sheria za Mungu.

Mwandishi mmoja alimwuliza Yesu swali. Andika maneno sawa katika mistari ya kifungu kifuatacho. Hili ndilo swali ambalo mwandishi huyo aliuliza:

"Katika _____ zote ni ipi iliyo ya _____?" (Marko 12:28)

Andika maneno sawa katika mistari hiyo hapo chini ili uweze kusoma jibu la Yesu kwa swali la mwandishi.

"Kwanza ndiyo hii, Sikia, _____, Bwana Mungu wetu ni _____; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa _____ wako wote, na kwa _____ yote, na kwa _____ zako zote, na kwa _____ zako zote." (Marko 12:29,30)

YESU AELEZA SHERIA ZA MUNGU

Andika maneno sawa katika mistari ya kifungu hiki kinachofuata. Hii ilikuwa amri ya pili ambayo Yesu alimwambia mwandishi.

"Mpende _____ kama _____
_____." (Marko 12:31)

Hapa kuna maswali mengine kwako kujibu juu ya somo la leo. Ikiwa ulisikiliza vyema, utaweza kujibu maswali haya yote.

Katika mwisho wa kila swali kuna maneno mawili. Chora mviringo kwa neno au maneno yanayojibu maswali.

1. Je! mwandishi alifikiri nini juu ya jibu la Yesu kwa swali lake?
(Alifurahi; hakufurahi)
2. Je! ni amri zipi katika Amri Kumi zinatwambia jinsi inavyotupasa kufikiri na kuonyesha matendo yetu kwa Mungu? (Amri nne za kwanza; Amri sita za kwanza)
3. Je! ni amri zipi katika Amri Kumi zinatwambia jinsi inavyotupasa kufikiri na kuonyesha matendo yetu kwa watu wengine? (Amri tatu za mwisho; amri sita za mwisho)
4. Je! Paulo alisema katika Warumi 13:10 kwamba ni kitu gani ambacho ni utimilifu wa sheria? (amani, upendo)

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Na amri hii tumepewa na yeye, ya kwamba yeye ampendaye Mungu, ampende na ndugu yake." 1 Yohana 4:21

Biblia inasema kwamba ukisema unampenda Mungu lakini unamchukia ndugu yako, u mwongo. Je! ulijua hivyo? Soma 1 Yohana 4:20. Kifungu hiki ndicho kinatangulia kifungu chako cha kukumbuka.

Paulo alisema kwamba upendo ndio utimilifu wa sheria zote za Mungu. Ni kwa sababu upendo hauwezi kumtendea mtu jambo lo lote baya. Je! unawapenda wengine kama unavyojipenda wewe mwenyewe?

Wakati mwingine ni ngumu kumpenda mtu aliyekukosea. Lakini Mungu anasema uwasamehe wale wanaokukosea na uwapende. Mwombe Mungu kukusaidia kuwapenda kama alivyokuamuru kupenda. Mwombe kukusaidia kuwasamehe wanaokukosea kama yeye alivyokusamehe. Ukiomba hivyo kwa moyo wako wote, na kwa imani, Mungu atajibu maombi yako.

MANENO YA KUJIFUNZA:

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Marko 12:28-34

Na mmojawapo wa waandishi akafika, akawasikia wakisemezana naye, akatambua

ya kuwa amewajibu vema, akamwuliza, Kati-
ka amri zote ni ipi iliyo ya kwanza? (29)
Yesu akamjibu, Ya kwanza ndiyo hii, Sikia
Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja;
(30) nawe mpende Bwana Mungu wako kwa
moyo wako wote, na kwa roho yako yote,
na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako
zote. (31) Na ya pili ndiyo hii, Mpende
jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri
nyingine iliyo kuu kuliko hizi. (32) Yule
mwandishi akamwambia, Hakika, Mwalimu,
umesema vema ya kwamba Mungu ni mmoja,
wala hakuna mwingine ila yeye; (33) na
kumpenda yeye kwa moyo wote, na kwa ufa-
hamu wote, na kwa nguvu zote, na kumpenda
jirani kama nafsi yako, kwafaa kuliko
sadaka nzima za kuteketezwa na dhahihu
zote pia. (34) Naye Yesu, alipoona kwamba
amejibu kwa busara, alimwambia, Wewe hu
mbali na ufalme wa Mungu. Wala hakuthu-
butu mtu kumsaili neno tena tokea hapo.

WAKATI TUNAPOKOSA KUTII SHERIA ZA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Waamuzi 14:1-15

Somo letu la leo ni juu ya wakati ambapo wana wa Israeli walikuwa wakita-waliwa na Wafilisti. Kulikuwa na mtu mmoja wa Israeli aliyeitwa Manoa. Yeye pamoja na mke wake walimpa Bwana na walitii sheria zake. Lakini hawakuwa na mtoto.


Siku moja Mungu aliwaambia kwamba wangepata mtoto mwanamume. Mtoto huyo angekuwa Mnadhiri. Mnadhiri ni mtu aliye-jitoa mwenyewe kwa Mungu kwa njia maalum. Hangekunywa divai, wala mvinyo, wala hangenyoa nywele zake. Nywele zake ndefu zingeonyesha kwamba yeye ni mtu wa Mungu.

Manoa na mke wake walipata mtoto kama Mungu alivyosema. Walimwita Samsoni. Walimfundisha habari za Mungu na sheria zake. Samsoni alikua, Mungu akambariki sana. Aliweka nadhiri yake. Alikuwa mtu mwenye nguvu nyingi.

Siku moja Samsoni alikwenda Timna, mji uliokuwa katika nchi ya Wafilisti. Wakati aliporudi nyumbani, aliwaambia baba yake na mama yake kwamba aliona mwanamke huko Timna ambaye alitaka kuoa.

Wazazi wake walimwuliza kwa nini hakutafuta mmojawapo wa mabinti wa Israeli kuwa mke wake. Lakini Samsoni alimta-ka mwanamke yule wa Timna kuwa mke wake.

Wazazi wa Samsoni walikwenda pamoja naye Timna kupanga ndoa. Wakati walipokuwa njiani, mwana-simba alimngurumia Samsoni katika mashamba ya mizabibu karibu na mji. Roho ya Bwana ilimjilia kwa nguvu. Alimpasua mwana-simba yule kana kwamba alikuwa akimpasua mwana-mbuzi. Alikuwa na nguvu nyingi!



Baadaye Samsoni alirudi Timna kwa ndoa yake. Aliona mzoga wa mwana-simba yule. Nyuki wengi walikuwamo ndani ya mzoga ule na asali. Alitwaa asali mikononi mwake, akala, akaenda zake.

Kulikuwa na Wafilisti thelathini katika karamu ya ndoa ya Samsoni. Aliwa-tegea kitendawili hiki: "Katika huyo mwenye kula kikatoka chakula, katika huyo mwenye nguvu ukatoka utamu." (Waamuzi 14:14)

Aliwaambia kwamba kama wangeweza kumwonyesha maana ya kitendawili hicho kabla karamu kwisha, angempa kila mmoja wao mavazi. Kama hawangeweza kumwonyesha, kila mmoja wao angempa mavazi.

Wafilisti walishindwa kupata jibu wenyewe. Walimwambia mke wa Samsoni kuwa-tafutia jibu. Mke wa Samsoni alilia, akamsihi Samsoni kumwambia jibu. Hatimaye Samsoni alimwambia jibu. Katika siku ya

saba ya karamu, Wafilisti walimwonyesha Samsoni maana ya kitendawili chake. Kisha alijua wazi kwamba mke wake ndiye aliye-waambia.

Samsoni alikwenda Ashkeloni, mji mwingine wa Wafilisti. Aliwaua watu the-lathini, akatwaa mavazi yao, akawapele-kea Wafilisti wale waliojibu kitendawili chake. Baadaye alimwacha mke wake Timna, akarudi nyumbani.

Wakati Samsoni aliporejea Timna kutembelea mke wake, alikuta kama mkwewe alimtoa mke wake kwa mume mwingine. Ali-kasirika sana. "Samsoni akaenda akakamata mbweha mia tatu; kisha akatwaa vienge vya moto akawafunga mbweha mkia kwa mkia, akatia kienge kati ya kila mikia miwili. Alipokwisha kuviwasha moto vile vienge, akawaachia mbweha kati ya ngano ya Wafilisti, akayateketeza matita, na ngano, hata na mashamba ya mizeituni." (Waamuzi 15:4-5)

Wafilisti waliwateketeza mke na mkwewe Samsoni kwa moto kwa sababu Samsoni aliteketeza mashamba yao. Kisha Samsoni aliwaua Wafilisti wengi sana kulipiza kisasi.

Siku nyingine tena Samsoni aliwaua Wafilisti elfu moja kwa mfupa wa taya ya punda. Alikuwa akitumia nguvu zake. Laki-ni alikuwa akitumia nguvu hizo kulipiza kisasi kwa maovu ambayo Wafilisti walimte-ndea.

Samsoni alifanya mapenzi na Delila, mwanamke mwingine Mfilisti. Wafilisti walikwisha kumwahidi Delila vipande elfu na mia moja vya fedha kama angeweza kuwambia asili ya nguvu za Samsoni.

Delila alimwomba Samsoni kumwambia asili ya nguvu zake. Samsoni alimdanganya mara tatu. Na katika mara hizo tatu Samsoni aliepuka kuuawa na Wafilisti wakati walipomfunga.

Delila aliendelea kumsihi Samsoni kumwambia asili ya nguvu zake. Mwishowe Samsoni alimwambia kwamba alikuwa Mnadhiri. Alisema ya kwamba kama angenyolewa hywele, nguvu zake zingemtoka. Delila alijua kwamba jambo hili lilikuwa kweli.

Wakati Samsoni alipokuwa akilala, Delila alimwita mtu mmoja kumnyoa Samsoni nywele. Kisha alipiga kelele, "Samsoni, Wafilisti wanakujia." (Waamuzi 16:20)


Samsoni aliamka akifikiri kwamba angeweza kuepuka kama alivyofanya nyakati zile zingine. Lakini Mungu alikuwa ameo-ndoa nguvu zake. Wafilisti walimkamata wakamng'oa macho. Walimfunga gerezani. Walimlazimisha kufanya kazi ngumu kuwasagia ngano. Lakini siku zilipoendelea kupita, nywele zake zilianza kukua tena baada ya kunyolewa kwake.

Siku moja, Wafilisti walimpeleka Samsoni katika hekalu lao. Watu wengi walikuja kumtolea sadaka Dagoni mungu wao. Walimweka Samsoni katikati ya hekalu

lao. Kulikuwa na watu zaidi ya elfu tatu ndani ya hekalu lile.

Samsoni alimwambia kijana aliyekuwa akimwongoza kumpeleka kwa nguzo zilizotegemeza hekalu lile. Kisha aliomba, "Ee Bwana Mungu, unikumbuke, nakuomba, ukaniatie nguvu, nakuomba, mara hii tu, Ee Mungu, ili nipate kujilipiza kisasi juu ya Wafilisti kwa ajili ya macho yangu mawili." (Waamuzi 16:28)

Samsoni alisukuma nguzo zile akisema, "Na nife pamoja na hawa Wafilisti." (Waamuzi 16:30a) Hekalu lile lilianguka



WAKATI TUNAPOKOSA KUTII SHERIA ZA MUNGU

na watu wote waliokuwamo ndani walikufa. Samsoni pia alikufa. Katika kifo chake, aliwaua Wafilisti wengi zaidi kuliko wale waliowaua wakati wa uhai wake.

Tunataka kuona jinsi Samsoni alivyo-kataa kumtii Mungu. Wakati Waisraeli walipokwenda Kanaani, Mungu aliwaambia kuwafukuza watu wote waliokaa pale kwa sababu watu hao hawakumwabudu.

Mungu aliwaambia Waisraeli kwamba watoto wao wasioe mabinti wa Kanaani. Samsoni alikataa kutii amri hii wakati alipooa mwanamke Mfilisti. Wazazi wake walimwuliza kwa nini hakutafuta binti mmoja wa Israeli kuoa. Alimwambia baba yake, "Mnipatie huyo, kwa maana ananipe-ndeza sana." (Waamuzi 14:3b)

Samsoni alikuwa mchoyo sana. Mambo mengi mabaya yalimpata maishani mwake kwa sababu alikataa kutii amri ya Mungu juu ya ndoa. Delila alikuwa mwanamke mwingine Mfilisti ambaye alimletea uchungu mwingi. Alimwambia Delila asili ya nguvu zake. Kisha Delila aliwaambia Wafilisti. Walimshika, wakamng'oa macho.

Mambo haya yote mabaya yalifanyika maishani mwa Samsoni kwa sababu alikataa kutii sheria za Mungu. Ni lazima tufahamu kwamba Mungu atatuadhibu sikuzote ikiwa tutakataa kumtii.

Ni lazima tuungame kutotii kwetu kwa Mungu. Tukifanya hivyo, Mungu atatusamehe. Lakini ni lazima tukumbuke kwamba Mungu

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

huwaadhibu watoto wake wanaokataa kumtii.

KAZI YA KUFANYA:

Katika hadithi yetu juu ya Samsoni, tumeona mambo yanayompata mtu wakati anapokataa kutii amri za Mungu. Neno la Mungu linatuambia wazi kwamba: "Msidanga-nyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna." (Wagalatia 6:7) Wakati mwingine unaweza kufanya jambo baya. Unafikiri kwamba hakuna mtu anayekuona au anayejua jambo hilo baya.

Hapa kuna vifungu vinavyotwambia kwamba hakuna kitu ambacho Mungu hawezi kukiona.

"...nanyi jueni ya kwamba hiyo dhambi yenu itawapata hapana budi." (Hesabu 32:23b)

"Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya." (Mhubiri 12:14)

"Lakini hakuna neno lililositirika ambalo halitafunuliwa, wala lililofichwa ambalo halitajulikana." (Luka 12:2)

Tusifikiri kwamba tunaweza kumficha Mungu jambo lo lote. Mungu anasikia mambo tunayosema. Anaona mambo yote tunayofanya. Anajua fikira zetu zote. Atatuadhibu sikuzote wakati tunapokataa kumtii. Lakini Mungu ni upendo. Daima hutusamehe

WAKATI TUNAPOKOSA KUTII SHERIA ZA MUNGU

wakati tunapomwomba kutusamehe. (Soma 1 Yohana 1:9.)

Hapa kuna sentensi juu ya maisha ya Samsoni. Andika herufi "K" katika mstari wa sentensi ya kweli, na uandike herufi "M" katika mstari wa sentensi ambayo si kweli.

1. Samsoni alikuwa mtoto wa kwanza wa wazazi wake. _____
2. Mungu aliwaambia wazazi wake kwamba atakuwa kuhani. _____
3. Mke wa kwanza wa Samsoni alikuwa Mfilisti. _____
4. Samsoni alimtii Mungu alipomwoa mwanamke Mfilisti. _____ (Soma Yoshua 23:11-13.)
5. Samsoni alipokuwa njiani kwenda Timna kwa ndoa yake, alingurumiwa na mwana-simba. _____
6. Roho ya Bwana alimjilia kwa nguvu. _____
7. Siku moja Samsoni aliwaua Wafilisti elfu moja kwa mfupa wa taya ya ng'ombe. _____
8. Samsoni alitumia nguvu zake daima kwa utukufa wa Mungu. _____
9. Delila alimdanganya Samsoni kwa hila ili Samsoni amwambie asili ya nguvu zake. _____

10. Wakati Samsoni alipokufa, aliwaua
Wafilisti wachache tu. _____

Jaza nafasi zilizoachwa katika kifun-
gu kifuatacho. Kifungu hiki kilikuwa
maombi ya mwisho ya Samsoni:

"Ee Bwana Mungu, _____, nakuomba,
ukanitie _____, nakuomba, mara hii
tu, Ee Mungu ili nipate _____
_____ juu ya Wafilisti kwa
ajili ya _____ yangu mawili."
(Waamuzi 16:28)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

*"Kwa maana mshahara wa dhambi ni
mauti; bali karama ya Mungu ni uzima
wa milele katika Kristo Yesu Bwana
wetu."
Warumi 6:23*

Inatupasa kufa kwa ajili ya dhambi
zetu. Lakini Mungu anatupa bure kipawa
chake cha uzima wa milele. Tukikataa
kipawa hiki chake cha uzima wa milele
kwa imani katika Mwanawe, Yesu Kristo,
basi tunachagua mauti.

Je! umekwisha kupokea kipawa cha
Mungu cha uzima wa milele? Ikiwa bado,
je! utachagua kumpokea Yesu leo? Fungua
moyo wako umkaribishe Yesu ndani. Anaku-
penda na anataka kukuokoa. Anataka kukupa
kipawa chake cha uzima wa milele.

MANENO YA KUJIFUNZA:

mnadhiri.....mtu anayeapa kutenda kitu.
mzoga.....mwili wa mnyama aliyekufa.

WAKATI TUNAPOKOSA KUTII SHERIA ZA MUNGU

taya.....mfupa wa kidevu.

asali.....namna ya maji matamu.

Ziko asali ya nyuki, ya
miwa na tembo.

kitendawili.....fumbo lenye maana mbili.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Waamuzi 14:1-15

Samsoni akatelemkia Timna, akaona mwanamke huko Timna, mmojawapo wa binti za Wafilisti. (2) Kisha akapanda, akawa-ambia baba yake na mama yake, akasema, Nimemwona mwanamke huko Timna, mmojawapo wa binti za Wafilisti; basi mnipatie, nimwoe. (3) Ndipo baba yake na mama yake wakamwambia, Je! hapana mwanamke hata mmoja katika ndugu zako, au katika jamaa zangu zote, hata uende kumwoa mwanamke kwa hawa Wafilisti wasiotahiriwa? Samsoni akamwambia baba yake; Mnipatea huyo, kwa maana ananipendeza sana. (4) Lakini baba yake na mama yake hawakujua ya kuwa jambo hili ni la BWANA; maana alitaka kisa juu ya Wafilisti. Basi wakati ule Wafilisti walikuwa wakiwatawala Israeli.

(5) Ndipo Samsoni na baba yake na mama yake wakatelemkia Timna, wakafika mashamba ya mizabibu huko Timna; na tazama, mwana-simba akamngurumia. (6) Roho ya BWANA ikamjilia kwa nguvu, naye akampasua kana kwamba anampasua mwana-mbuzi, wala hakuwa na kitu cho chote mkononi mwake; lakini hakuwaambia baba yake na mama yake aliyoyafanya. (7) Basi akatelemka na kuzungumza na huyo mwanamke; naye akampe-ndeza Samsoni sana. (8) Kisha baadaye akarudi ili kumtwaa, naye akageuka kando kuuangalia mzoga wa huyo simba; na tazama,

nyuki wengi walikuwamo ndani ya mzoga wa simba, na asali. (9) Akatwaa asali mikononi mwake, akaenda mbele, huku akila alipokuwa akienenda, akawafikilia babaye na mamaye, akawapa, nao wakala; lakini hakuwaambia ya kuwa ameitwaa hiyo asali katika mzoga wa simba. (10) Basi babaye akamtelemkia huyo mwanamke; Samsoni naye akafanya karamu huko; kwa kuwa vijana ndivyo walivyokuwa wakifanya. (11) Basi ikawa hapo walipomwona, wakamletea wenziwe thelathini, wawe pamoja naye. (12) Samsoni akawaambia, Mimi nitawategea ninyi kitendawili; kama mwaweza kunionyesha katika hizo siku saba za karamu, na kukitambua, ndipo hapo nitawapa mavazi thelathini ya kitani na mavao mengine thelathini; (13) lakini msipoweza kuni-onyesha ndipo hapo ninyi mtanipa mimi mavazi thelathini ya kitani na mavao mengine thelathini. Basi wakamwambia, Haya, tega kitendawili chako, ili tupate kukisikia. (14) Naye akawaambia, Katika huyo mwenye kula kikatoka chakula, Katika huyo mwenye nguvu ukatoka utamu. Nao katika siku tatu hawakuweza kukifungua hicho kitendawili. (15) Ikawa kwa siku ya saba, wakamwambia mkewe Samsoni, Mbembeleze mumeo, ili atuonyeshe hicho kitendawili, tusije tukakuteketeza moto wewe na nyumba ya baba yako; je! mmetuita ili mpate kuichukua mali yetu? je! sivyo?

NJIA YA KUWA NA FURAHA

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo 3:1-15


Hapo mwanzo Mungu aliumba ulimwengu. Alipanda bustani nzuri iliyoitwa bustani ya Edeni. Aliwaumba mume na mke kwa mfano wake. Waliitwa Adamu na Hawa. Aliwaweka katika bustani ya Edeni kuilima na kuitunza.

Mungu alipanda miti katika bustani ya Edeni. Miti mingi ilikuwa ya kupendeza macho. Miti mingi ilikuwa na matunda mema ya kula. Katikati ya bustani Mungu alipanda mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Kulikuwa na mto katika Edeni wa kuitilia bustani maji.

Mungu alimwambia Adamu, "...Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, wala-kini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika."
(Mwanzo 2:16, 17)

Adamu na Hawa walikuwa na furaha katika makao yao mema bustanini. Kisha jambo fulani lilifanyika, likaondoa furaha yao.

Siku moja, Shetani katika umbo la nyoka alikuja kumjaribu Hawa. Alimwambia, "...Ati! hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?"
(Mwanzo 3:1)



Siku moja, Shetani katika umbo la nyoka alikuja kumjaribu Hawa. Alimwambia, "...Ati! hivi ndivyo alivyo-sema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?" (Mwanzo 3:1)

Hawa alimjibu, "...Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula;

lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa." (Mwanzo 3:2,3)

Lakini Shetani alimwambia Hawa, "...Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakapokula matunda ya mti huo mtafumbuliwa macho, nanyi mta-kuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya." (Mwanzo 3:4,5)

Kisha Shetani alimfanya Hawa kuona jinsi matunda ya mti ule yalikuwa ya kutamanika kula. Alimfanya Hawa kufikiri jinsi kula matunda hayo kungekuwa kuzuri. Hata alimfanya Hawa kufikiri kwamba lingekuwa jambo jema kwake kula matunda ya mti ule ili angeweza kujua mema na mabaya. Hawa alitwaa matunda yale, akala. Kisha alimpa Adamu mengine, naye akala.

Mara tu baada ya Adamu na Hawa wali-pokula matunda ya mti ule waliokatazwa na Mungu, walijijua kuwa walikuwa uchi. Walishona majani ya mtini, wakajifanyia nguo.

Adamu na Hawa walisikia sauti ya Bwana Mungu akitembea bustanini wakati wa jua kupunga upepo. Walijificha.

Mungu alimwita Adamu, akamwambia, "Uko wapi?" (Mwanzo 3:9b)

Adamu alisema, "Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha." (Mwanzo 3:10)

Kisha Mungu aliwauliza kama walikula matunda ya mti aliowakataza. Adamu alisema kwamba Hawa ndiye aliyempa matunda ya mti ule, akala.

Hawa alimlaumu Shetani. Alisema kwamba alidanganywa na Shetani, akala matunda ya mti ule aliokatazwa.

Udhuru waliotoa haukuwasaidia. Mungu aliwafukuza katika bustani. Walichagua kutomtii Mungu. Walistahili adhabu ya kifo ambacho Mungu aliwaonya juu yake. Kifo hiki maana yake kutengwa milele na Mungu. Tumaini lao pekee lilikuwa kwa Mungu kuwapa njia ya kusamehewa dhambi yao.

Mungu aliwapenda Adamu na Hawa. Aliwapenda hata baada ya wao kutenda dhambi. Lakini ilikuwa lazima kuwaadhibu kwa

ajili ya dhambi yao kama Mungu alivyo-sema. Mungu aliwapa uchaguo. Lakini wao walichagua kukataa kutii amri yake.

Mungu alimfanyia mwanadamu njia ya kusamehewa dhambi. Alimtuma Mwanawe Yesu Kristo kufa msalabani kwa ajili ya dhambi ya kila mmoja wetu. Biblia inasema, "...wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." (Warumi 3:23) Pia, Biblia inasema kwamba mshahara wa dhambi ni mauti. (Soma Warumi 6:23.)

Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu ili sisi tusife kwa ajili ya dhambi hizo. Lakini ni lazima tuchague kumwamini. Ni lazima tutambue kwamba sisi ni wenye dhambi wanaostahili kufa kwa ajili ya dhambi zetu.

Kisha ni lazima tuungame dhambi zetu kwa Mungu na kumwamini Yesu kama Mwokozi wetu. Alikufa ili tupate kuishi. Una uhu-ru kuchagua. Unaweza kuchagua wewe mwenye-we kumfuata.

Je! umekwisha kumchagua Yesu kama Mwokozi wako? Ikiwa umekwisha kufanya hivyo, una uzima wa milele. Je! ikiwa bado, utafanya hivyo leo? Yesu anataka kukupa maisha ya milele. Hataki ufe kwa ajili ya dhambi zako.

Njia ya kuwa na furaha halisi ni kumpenda Mungu na kutii amri zake. Katika somo letu lililopita tulijifunza jinsi Samsoni alivyopatwa na shida nyingi kwa sababu hakutii amri za Mungu. Kutotii,

sikuzote huleta hali ya kutokuwa na furaha.

Kutii amri za Mungu peke yake hakuwezi kutuokoa. Kumwamini Yesu Kristo ndiyo inayotuokoa. Uzima wa milele ni kipawa kutoka kwa Mungu. Lakini kutii amri za Mungu kutatupa furaha. Hatuwezi kufurahi tusipomtii Mungu kwa sababu dhambi yetu inatuzuia kuwa na ushirika naye.

Kumtii Mungu ndiyo njia ya furaha. Mwombe Mungu kukusaidia kuwa mtiifu. Jifunze Neno la Mungu ili uweze kujua kujua jinsi ya kuwa mtiifu. Weka Neno la Mungu moyoni mwako ili usimtende dhambi.

KAZI YA KUFANYA:

Wakati Mungu alipomwumba mwanadamu, alimpa kila kitu kumfurahisha. Alimpa mahali pema sana pa kukaa. Mungu alimpa mwanadamu uhuru wa kuchagua.

Jibu maswali yafuatayo juu ya mambo yaliyowafanyikia Adamu na Hawa katika makao yao mapya.

1. Je! Mungu alipanda mti gani kati-kati ya bustani? _____
2. Je! Mungu aliwapa Adamu na Hawa amri gani juu ya mti ule? _____
3. Je! Shetani alimjia Hawa katika umbo la mnyama gani? _____

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

4. Je! Shetani alimpa Hawa sababu gani kwamba ale matunda ya mti ule uliokuwa katikati ya bustani?

5. Je! Baada ya Hawa kula matunda alifanya nini? _____
6. Baada ya Adamu na Hawa kula matunda, walisikia sauti ya Bwana Mungu akitembea bustanini. Je! walifanya nini? _____
7. Je! Mungu aliwafanyia Adamu na Hawa jambo gani baada ya wao kukataa kumtii? _____
8. Mungu alitufanyiaje njia ya kusamehewa dhambi zetu? _____
9. Je! kutii amri za Mungu peke yake kunatuokoa? _____
10. Je! tunaweza kuokolewa kwa njia gani? _____

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Pasipo maono, watu huacha kujizuia; bali ana heri mtu yule aishikaye sheria." *Mithali 29:18*

Kifungu hiki chetu cha kukumbuka kinatwambia kwamba tutafurahi kama tutashika sheria za Mungu. Mwombe Mungu kukusaidia kuwa mtiifu na kumfuata Yesu kama mwanafunzi wake wa kweli.

MANENO YA KUJIFUNZA:

kupunga.....kujongea huko na huko.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mwanzo 3:1-15

Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya BWANA Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani? (2) Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustani twaweza kula; (3) lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. (4) Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamta-kufa, (5) kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya. (6) Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala. (7) Wakafumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo. (8) Kisha wakasikia sauti ya BWANA Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, BWANA Mungu asiwaone. (9) BWANA Mungu akamwita Adamu, akamwambia, Uko wapi? (10) Akasema, Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha. (11) Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza

usiyale? (12) Adamu akasema, Huyo mwana-
mke uliyenipa awe pamoja nami ndiye ali-
yenipa matunda ya mti huo, nikala. (13)
BWANA Mungu akamwambia mwanamke, Nini
hili ulilolifanya? Mwanamke akasema, Nyoka
alinidanganya, nikala. (14) BWANA Mungu
akamwambia nyoka, Kwa sababu umeyafanya
hayo, umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote,
na kuliko hayawani wote walioko mwituni;
kwa tumbo utakwenda, na mavumbi utakula
siku zote za maisha yako; (15) nami nita-
weka uadui kati yako na huyo mwanamke, na
kati ya uzao wako na uzao wake; huo utaku-
ponda kichwa, na wewe utamponda kisigino.

KIPAWA KIKUU

MASOMO YA BIBLIA: Luka 2:1, 4-18

Hapa kuna swali kutoka somo letu lililopita. Je! ni kwa nini Mungu aliwafukuza Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni? Ndiyo, kwa sababu hawakutii amri ya Mungu. Kifo ndicho kilikuwa adhabu ya kutotii kwao. Je! kifo hicho kilikuwa cha aina gani? Kilikuwa mtengano milele na Mungu. Kutoka wakati ule wa Adamu na Hawa, watu wamekuwa wakitenda dhambi na wanastahili kufa.

Mungu aliwapenda watu alioumba. Aliahidi kumtuma Mwanawe kuwafanyia watu wote njia kuwa watoto wake. Kipawa kikuu cha Mungu kwa ulimwengu kilikuwa Mwanawe Yesu Kristo.

Tunapomwamini Yesu tunakuwa watoto wa Mungu. Tunaweza kuwa na ushirika wa ajabu na Baba yetu aliye mbinguni kwa sababu Yesu alikuja ulimwenguni kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Yesu ndiye njia, na kweli, na uzima. (Soma Yohana 14:6.)

Katika wakati huu wa Krismasi, tufikirie tena wakati ule ambapo Yesu alikuja ulimwenguni.

Watu walimtazamia Mwokozi, Mwana wa Mungu kuja kwa muda wa miaka mingi sana. Akina mama na akina baba waliwaambia watoto zao habari za Mwokozi aliyeahidiwa kuja. Mungu aliwaambia manabii jinsi Yesu angezaliwa Bethlehemu. Hatimaye wakati

ulifika kwa Yesu, Mwana wa Mungu, kuza-liwa.

"Siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augusto ya kwamba iandikwe orodha ya majina ya watu wote wa ulimwengu."
(Luka 2:1)

Wakati huu Yusufu alikuwa akikaa Nazareti, lakini Bethlehemu ndio uliokuwa mji wao. Alimchukua Mariamu, wakaenda Bethlehemu kuandikwa majina.

Wakati walipokuwa Bethlehemu, siku ya Mariamu kuzaa mtoto ilitimia. Yesu Kristo Mwana wa Mungu alizaliwa katika zizi la ng'ombe kwa sababu hapakuwa na nafasi katika nyumba ya wageni. Mambo ambayo Mungu aliwaambia mitume miaka mingi iliyopita, sasa yalitimia.

Mariamu alimchukua mtoto Yesu, aka-mvika nguo za kitoto. Alimlaza katika hori ya kulia ng'ombe.

Kulikuwa na wachungaji wakikaa mako-ndeni kulinda kondoo zao usiku. Malaika wa Bwana aliwatokea kwa ghafula. Utukufu wa Bwana uliwang'aria pande zote. Walio-gopa sana.

"Malaika akawaambia, Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaleteta habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana." (Luka 2:10,11)

Mara walikuwapo pamoja na malaika huyo wingi wa jeshi la mbinguni. Walikuwa wakimsifu Mungu wakisema, "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia." (Luka 2:14)

Wakati malaika hao walipoondoka kwenda zao mbinguni, wachungaji walijiha-rakisha kwenda Bethlehemu kuona jambo hilo waliloambiwa na Bwana. Walipofika, walimkuta Mariamu na Yusufu zizini. Mtoto Yesu alikuwa amelazwa katika hori ya kulia ng'ombe.



Wachungaji walipokuwa wakirejea, walimsifu na kumtukuza Mungu kwa mambo yote waliyoona na kusikia. Waliwasikia malaika wakiimba wimbo ambao unapasa uli-mwengu wote kuusikia!

Je! umekwisha kupokea kipawa kikuu cha Mungu ambaye ni Mwanawe Yesu Kristo, kuwa Mwokozi wako? Ikiwa umekwisha kumpokea, basi wewe pia unaweza kumsifu na

kumtukuza Mungu kwa mambo ambayo amekwisha kupa.

Wachungaji walitoa habari juu ya mambo waliyoona na kusikia. Wewe je? Je! ikiwa wewe ni Mkristo, utamwambia mtu mwingine habari za upendo wa Mungu? Utaeleza kwamba Yesu ambaye ni kipawa kikuu cha Mungu alikuja ulimwenguni kufa ili tuweze kupata uzima wa milele?

Je! ikiwa bado hujamwamini Yesu kukuokoa, utafanya hivyo leo? Mungu anakupenda na anataka upokee kipawa chake kikuu, Yesu Kristo kuwa Mwokozi wako.



KAZI YA KUFANYA:

Hadithi yako leo, labda ni hadithi unayoifahamu vyema. Lakini kujua kwamba kuna watu wengi ulimwenguni ambao hawajasikia hadithi hii ya ajabu juu ya Yesu kunahuzunisha sana.

Krismasi ni wakati wa kushiriki. Jaribu kupata mtu aliye katika hali ya ukiwa, anayehitaji kupendwa. Je! unamfahamu mtu ye yote mgonjwa anayehitaji kusaidiwa? Unamjua mtu ye yote anayehitaji chakula?

Labda wanafunzi wa darasa lako watakwenda pamoja kumtendea mtu ye yote mwe-nye hitaji jambo jema. Lakini jambo muhimu sana unaloweza kufanya ni kushiriki hadithi ya Yesu kama Mwokozi wa ulimwe-ngu.

Hapa kuna sentensi juu ya mambo yaliyofanyika katika hadithi yako ya leo. Andika namba katika mistari iliyo kando ya sentensi hizo kulingana na wakati zilipofanyika.

Labda wanafunzi wa darasa lako watakwenda pamoja kumtendea mtu ye yote mwe-nye hitaji jambo jema. Lakini jambo muhimu sana unaloweza kufanya ni kushiriki hadithi ya Yesu kama Mwokozi wa ulimwe-ngu.

Hapa kuna sentensi juu ya mambo yaliyofanyika katika hadithi yako ya leo. Andika namba katika mistari iliyo kando ya sentensi hizo kulingana na wakati zilipofanyika.

— Yusufu alimchukua Mariamu Bethlehemu kuandikwa majina yao.

— Mungu aliwaambia mitume jinsi Yesu angezaliwa Bethlehemu.

— Malaika wa Bwana aliwatokea wachungaji makondeni.

— Wakati Yusufu na Mariamu walipo-kuwa Bethlehemu siku za Yesu kuzaliwa zilitimia.

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

- Jeshi la mbinguni waliimba pamoja na malaika yule.
- Mariamu alimvika mtoto Yesu nguo za kitoto, akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe.
- Wachungaji walikwenda kwa haraka Bethlehemu kuona jambo lile ambalo Bwana aliwaambia.
- Jeshi la mbinguni waliimba, "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duni-ani iwe amani kwa watu aliowaridhia." (Luka 2:14)
- Wachungaji walirudi wakimsifu na kumtukuza Mungu kwa mambo yote waliyoona na kusikia.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."
Yohana 3:16

Kifungu hiki cha kukumbuka ni cha thamani kuu. Je! unakijua kwa moyo? U tajiri sana moyoni ikiwa unamwamini Yesu. Wewe kama mwamini, una uzima wa milele. Siku moja utakaa pamoja na Mungu katika makao yako mbinguni ambayo amekwisha kuwatayarishia watoto wake wote.

Mwombe Mungu kukusaidia kushiriki habari njema ya wokovu na marafiki zako

wote. Wakati huu wa Krismasi ambapo unafikiria upendo wa Mungu, umwombe Mungu kuku-saidia kuwa mtu ambaye kweli anawapenda wengine.

MANENO YA KUJIFUNZA:

ukiwa.....ukame, upweke, hali ya
kufiwa.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Luka 2:1, 4-18

Siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augusto ya kwamba iandikwe orodha ya majina ya watu wote wa ulimwengu. (4) Yusufu naye aliondoka Galilaya, toka mji wa Nazareti, akapanda kwenda Uyahudi mpa-ka mji wa Daudi, uitwao Bethlehemu, kwa kuwa yeye ni wa mbari na jamaa ya Daudi; (5) ili aandikwe pamoja na Mariamu mkewe, ambaye amemposa, naye ana mimba. (6) Ika-wa, katika kukaa huko, siku zake za kuzaa zikatimia, (7) akamzaa mwanawe, kifungua mimba, akamvika nguo za kitoto, akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni.

(8) Na katika nchi ile ile walikuwako wachungaji wakikaa makondeni na kulinda kundi lao kwa zamu usiku. (9) Malaika wa Bwana akawatokea ghafula, utukufu wa Bwana ukawang'aria pande zote, wakaingiwa na hofu kuu. (10) Malaika akawaambia, Msio-gope; kwa kuwa mimi ninawaleteta habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; (11) maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana. (12) Na hii ndiyo ishara

BIBLIA, KITABU CHA DAIMA

kwenu; mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ng'ombe. (13) Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema,

(14) Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowari-dhia. (15) Ikawa, malaika hao walipoondoka kwenda zao mbinguni, wale wachungaji wali-ambiana, Haya, na twendeni mpaka Bethlehe-mu, tukalione hilo lililofanyika, alilotu-julisha Bwana. (16) Wakaenda kwa haraka wakamkuta Mariamu na Yusufu, na yule mtoto mchanga amelala horini. (17) Walipomwona wakatoa habari waliyoambiwa juu ya huyo mtoto. (18) Wote waliosikia wakastaajabu kwa hayo waliyoambiwa na wachungaji.

TUNU ZANGU KWA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Mathayo 2:1-12

Je! umepata kutazama nyota mbinguni usiku? Je! zinajongea? Watu wengine huta-zama nyota kwa uangalifu sana. Wanajua mengi juu yao. Somo hili letu la leo ni juu ya watu wengine waliofuata nyota iliyowaongoza.

Wakati Yesu alipozaliwa katika Beth-lehemu ya Uyahudi, mamajusi wengine kuto-ka mashariki walikuja Yerusalemu. Herode ndiye aliyekuwa mfalme wakati ule. Mama-jusi wale walikuwa wakiuliza, "Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia." (Mathayo 2:2)


Mfalme Herode alifadhaika sana alipo-sikia maneno hayo ya mamajusi. Kila mtu katika Yerusalemu alifadhaika. Herode aliwaita wakuu wa makuhani na waandishi. Aliwauliza kwamba Kristo alizaliwa wapi. Walimwambia mambo yaliyoandikwa na mana-bii juu ya Yesu.

Nabii Mika alitoa unabii wake akise-ma: "Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja ataka-yekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele." (Mika 5:2)

Kisha Herode aliwapelekea mamajusi umbe wake kwake. Aliwauliza muda walipo-

iona nyota ile. Aliwaambia waende wakaulize sana mambo ya mtoto yule. Alisema, "...mkiisha kumwona, nileteeni habari, ili mimi nami niende nimsujudie."
(Mathayo 2:8)

Mamajusi walipokwisha kumsikia mfalme Herode, walikwenda zao. Wakati walipokuwa wakisafiri, waliona nyota ile ile waliyoiona mashariki. Iliwatangulia mpaka



ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto Yesu.

Mamajusi walifurahi sana walipoiona nyota ile. Waliingia nyumbani, wakamwona mtoto Yesu pamoja na Mariamu mamaye. Je! umeona kwamba Biblia inasema mtoto Yesu alikuwa ndani ya nyumba, siyo zizini wakati huu? Labda alikuwa na umri zaidi

TUNU ZANGU KWA MUNGU

ya mwaka mmoja wakati ambapo mamajusi walimwona.

Mamajusi walipoingia nyumbani, alianguka, wakamsujudia Yesu. Walimtolea tunu za dhahabu na uvumba na manemane. Tunu hizi zilikuwa za thamani nyingi sana. Walimtolea tunu, zao nzuri sana kuliko nyingine zote walizokuwa nazo.

Lakini kabla mamajusi wale kumtolea Yesu tunu zao, walianguka, wakamsujudia. Tunu yao ya kwanza kwa Yesu ilikuwa ibada yao.

Je! ni kitu gani unachoweza kumpa Mungu ambacho kitampendeza zaidi kuliko kitu cho chote? Katika somo la tisa la kitabu hiki tulijifunza juu ya jibu la Yesu kwa swali lililouliza, "...Katika amri zote ni ipi iliyo ya kwanza?" (Marko 12:28) Je! jibu hilo la Yesu lilikuwa lipi? Ikiwa hulikumbuki, utazame tena somo la tisa.

Ndiyo, Mungu anataka tumpende kwa mioyo yetu yote, kwa roho zetu zote, kwa akili zetu zote, na kwa nguvu zetu zote. Je! unampenda Mungu kama hivyo?

Katika somo lililopita tulijifunza juu ya kipawa cha Mungu cha upendo kwetu. Ni upendo mkuu! Alitupa Mwanawe, Yesu. Leo tunafikiri juu ya zawadi yetu kwake. Anataka ibada na upendo wetu. Anataka maisha yetu.

Je! ukiwa bado kumtolea upendo na maisha yako, utafanya hivyo sasa? Atapezwa sana na vipawa kama hivyo!

KAZI YA KUFANYA:

Hapa kuna maswali juu ya somo lako la leo. Andika jibu sawa katika mstari wa kila sentensi.

1. _____ ndiye aliyekuwa mfalme wa Yerusalemu wakati Yesu alipozaliwa Bethlehemu.
2. Mamajusi walitoka _____.
3. Mamajusi walikuwa wakiuliza, "Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa _____...?" (Mathayo 2:2)
4. Herode _____ sana wakati aliposikia maneno ya mamajusi.
5. Herode aliwaambia mamajusi kwamba wakiisha kumwona mtoto Yesu wamletee habari. Alisema kwamba yeye pia alitaka kwenda _____.
6. Mamajusi walifuata _____ mpaka mahali mtoto Yesu alipokuwa.
7. Walimtolea tunu za _____, _____, na _____.
8. Kabla mamajusi kumtolea Yesu tunu zao, walianguka, _____.

TUNU ZANGU KWA MUNGU

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"...kwanza walijitoa nafsi zao kwa
Bwana; na kwetu pia, kwa mapenzi ya
Mungu." 2 Wakorintho 8:5

Kitu muhimu sana unachoweza kumtolea
Mungu ni maisha yako. Mungu anataka umpe-
nde na umtolee moyo wako kwanza. Kisha
unapompenda, utamttoa vipawa au tunu
zako.

Je! umekwisha kutoa nafsi yako kwa
Mungu? Hiyo ndiyo tunu ya ajabu kumtolea
Yesu wakati huu wa Krismasi.

MANENO YA KUJIFUNZA:

tunu.....hedaya, kitu cha thamani,
zawadi.
mamajusi.....watu wenye elimu ya nyota.
zizi.....ua, banda, n.k. cha kuwe-
kea mifugo.
hori.....birika la kunywea maji
wanyama.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mathayo 2:1-12

Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu
ya Uyahudi zamani za mfalme Herode,
tazama, mamajusi wa mashariki walifika
Yerusalem, wakisema, (2) Yuko wapi yeye
aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa
maana tuliona nyota yake mashariki, nasi
tumekuja kumsujudia. (3) Basi mfalme
Herode aliposikia hayo, alifadhaika, na
Yerusalem pia pamoja naye. (4) Akakusa-

nya wakuu wa makuhani wote na waandishi wa watu, akatafuta habari kwao, Kristo azaliwa wapi? (5) Nao wakamwambia, Katika Bethlehemu ya Uyahudi; kwa maana ndivyo ilivyoandikwa na nabii, (6) Nawe Bethlehemu, katika nchi ya Yuda, Hu mdogo kamwe katika majumbe wa Yuda; Kwa kuwa kwako atatoka mtawala Atakayewachunga watu wangu Israeli.

(7) Kisha Herode akawaita wale mama-jusi faraghani, akapata kwao hakika ya muda tangu ilipoonekana ile nyota. (8) Akawapeleka Bethlehemu, akasema, Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya mtoto; na mkiisha kumwona, nileteeni habari, ili mimi nami niende nimsujudie. (9) Nao waliposikia maneno ya mfalme, walishika njia; na tazama, ile nyota waliyoiona mashariki ikawatangulia, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto. (10) Nao walipoiona ile nyota, walifurahi furaha kubwa mno. (11) Wakaingia nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia; nao walipokwisha kufungua hazina zao, wakamtolea tunu; dhahabu na uvumba na manemane. (12) Nao wakiisha kuonywa na Mungu katika ndoto wasimrudie Herode, wakaenda zao kwao kwa njia nyingine.

BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE

AN AGENCY OF THE BAPTIST MISSION OF EAST AFRICA
TELEPHONE 52744 - P. O. BOX 30376 - NAIROBI, KENYA

